Jumatano Agosti 19, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580314

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710



## NEC yataka wananchi kuheshimu sheria kuelekea uchaguzi mkuu

UKURASA 3




UKURASA 11

# RC atoa neno msafara wa mgombea kushambuliwa

UKURASA 2



Baadhi ya wananchi waliodai ni wanachama wa CCM kutoka kata kadhaa za Jiji la Dodoma, wakiwa nje ya ofisi za chama hicho, Wilaya ya Dodoma Mjini jana, wakilalamikia baadhi ya wagombea, walioongoza kura za maoni za udiwani kuenguliwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# WB kuimwagia Tanzania tril.1/- ujenzi sekondari

UKURASA 2

## SERIKALI KUNUNUA MAHINDI YA WAKULIMA

UKURASA 3

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhele (katikati), akimpongeza Mkurugenzi Mtendaji mpya wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, baada ya kuthibitishwa kwenye nafasi hiyo jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mjumbe wa Bodi ya benki hiyo, Margareth Ikongo. Habari Uk. 8. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store

MICHEZO **KOCHA MPYA YANGA MZIGONI KIMYA KIMYA** UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa ya Halmashauri Kuu ya CCM na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiteta jambo na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Job Ndugai (kulia) na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid kabla ya kuanza kwa Kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama hicho, katika Ikulu ya Chamwino Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# RC atoa kauli msafara wa mgombea kushambuliwa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amezungumzia tukio la kushambuliwa kwa mawe wilayani Hai mkoani Kilimanjaro kwa msafara wa mmoja wa wagombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, akisema hakukuwa na sababu na uhalali wowote wa kufanyika kwa kitendo hicho.

Mghwira alitoa kauli hiyo jana alipojibu hoja iliyotolewa na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, aliyezungumzia tukio hilo wakati wa Mkutano Mkuu wa 36 wa Dayosisi ya Kaskazini, akitaka jambo hilo kukemewa.

Wakati anatoa salamu za serikali, Mghwira alisema: "Na ni kweli juzi Ijumaa, ninakiri alipita hapa mgombea mmoja, na katika Jimbo letu la Hai vijana pale wakaanzisha vurugu.

"Lakini, baadaye nilipata taarifa jioni niliporudi, kwa sababu nilikuwa Same, niliambiwa kwamba yuko Arusha, lakini alipofika Hai kulitokea tatizo ambalo vijana walianza kutupiana mawe kweli bila sababu.

"Hakukuwa na sababu yoyote, wala hakukuwa na uhalali wowote, lakini hilo nitalisemea mahali panapotakiwa. Ninaomba tu kanisa litambue kwamba tumeona hitilafu hiyo iliyojitokeza, tumeifanyia kazi na mimi nitaitolea maelezo hivi karibuni."

**KAULI YA DK. SHOO**

Katika hotuba yake wakati anafungua mkutano huo, Dk. Shoo alisema: "Kipekee nimesikitishwa sana na vitendo ambavyo vinafanywa na vijana wahuni wachache, na sijajua nani anayewaongoza kushambulia mikutano ya wale ambao wanapita kutafuta wadhamini.

"Jambo hili linafaa kukemewa kwa sababu huo ni mwanzo, ni jambo la hatari ambalo linaweza likaleta shida na kuvuruga amani. Kwa ajili hiyo, niwaombe sana kwa pamoja na kwa nia njema kabisa, tukemee vitendo vya namna hiyo.

"Tukumbuke kwamba amani ni tunda la haki na uonevu unapokithiri na haki kukanyagwa, amani inaweza ikatoweka. Na hili linaweza likawa jambo la kufumba na kufumbua."

Kiongozi huyo wa kanisa pia alisisitiza kuwa Watanzania wanapaswa kujifunza kwa nchi jirani madhara ya vitendo vya aina hiyo hasa nyakati kama hizi za uchaguzi au baada ya uchaguzi.

"Mungu atunusuru ili lisitokee kwetu na sisi tusiwe sehemu ya visababishi. Ninawahimiza wakristo na watu wote, Watanzania wenzangu kushiriki kwa haki, kushiriki usawa, uwazi, amani na utulivu katika machakato wa kuwapata viongozi bora, ili tusije tukafika mahali tukalalamika na kujutia kwamba kumekuwa na viongozi waovu.

"Wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu, sikilizeni wagombea ili upate ufahamu kama ana sifa sahihi za kiongozi bora na kufanya uchaguzi sahihi siku ya uchaguzi.

"Ni kweli huwa sisi viongozi wenu, viongozi wa dini hatupaswi kuwa washabiki wa chama fulani, lakini ni wajibu wetu kuwasaidia watu kupata ujuzi wa kweli kuhusu mtu anayefaa kuwa kiongozi," Dk. Shoo alisema.

Askofu huyo pia aliwataka viongozi wa kanisa hilo na waumini wake kushirikiana na serikali na vyombo vingine vyote vya kusimamia uchaguzi mkuu na watu wengine wote wenye mapenzi mema.

Alisema kuwa wao wanaendelea kusisitiza Watanzania wanao wajibu wa kuchagua watu wafaao kuongoza na wala siyo chama.

"Tuangalie sana watu waadilifu, watu wacha Mungu, wenye nia ya dhati ya kuwatumikia Watanzania. Sisi Dayosisi ya Kaskazini tunapenda kuwahimiza Watanzania kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi huu.

"Tunapenda kutoa rai kwa wana dayosisi na jamii kwa ujumla, kuzingatia maadili mema kama kigezo kikuu cha kuwachagua viongozi wetu.

"Tunawasihi sana wanasiasa, viongozi wenzangu wa dini zote na Watanzania kwa ujumla, tudumishe haki, tudumishe amani na utulivu, kwani hizi ni tunu za pekee katika maisha ya taifa letu. Mkumbuke kwamba tunu ya ama-

# Serikali, WB kutekeleza mradi wa tril. 1/- kuboresha elimu sekondari

**Na Salome Kitomari**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), imesema itatekeleza mradi wa miaka mitano wa kuinua ubora wa elimu ya sekondari nchini, wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 500 (zaidi ya trilioni moja).

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa wadau elimu kujenga uelewa wa pamoja kuhusu mradi wa kuinua ubora wa elimu ya sekondari (SEQUIP), uliofadhiliwa na Benki ya Duniani (WB), alisema mradi huo utaleta mabadiliko ya uendeshaji wa shule za sekondari nchini na kuondoa changamoto zinazoikabili sekta ya elimu.

Alisema mradi huo utanufaisha wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita milioni 6.5, wakiwamo wasichana milioni 3.2.

Mkutano huo ulijumuisha wadau kutoka sekta binafsi, maofisa elimu mikoa, wathibiti ubora wa shule kanda, wakuu wa vyuo vya maendeleo ya wananchi, wakuu wa shule, Maofisa Wizara ya Elimu na TAMISEMI, pamoja na washirika wa maendeleo wa nchi mbalimbali duniani waliofuatilia kwa mtandao.

Akifungua mkutano huo, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilipo, alisema katika kipindi cha miaka mitano serikali ilijikita katika ujenzi wa miundombinu ya shule za sekondari na msingi.

Alisema katika utekelezaji wa mpango wa elimu bila ada, wanafunzi wengi wanatarajiwa kumaliza shule za msingi na hakuna miundombinu ya kutosha sekondari.

"Ongezeko la wanafunzi litaonekana katika shule za sekondari miaka mitatu kuanzia sasa na kuwa na hitaji la miundombinu mara dufu ya iliyopo sasa, na namna ya kukabiliana nalo utekelezaji mradi wa kuinua ubora wa elimu ya sekondari," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Akwilipo, mradi huo umelenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, ujenzi wa shule mpya 1,000 kila moja yenye uwezo wa kubeba wanafunzi 400 katika halmashauri mbalimbali.

Pia, zitajengwa shule mpya za kisasa kila mkoa kwa ajili ya wanafunzi wasichana watakaochukua masomo ya sayansi, kuendesha mafunzo kazini kwa walimu wa Sayansi, Hisabati na lugha zaidi ya 20,000.

Alisema pia shule 50 kongwe zitakarabatiwa, kumalizia ujenzi na ukarabati wa maabara na kuwasaidia wanafunzi wa kike walioshindwa kumaliza shule kwa sababu mbalimbali kuendelea na elimu.

Shule kongwe 50 zitakarabatiwa, kukarabati na kumaliza maabara zote nchini kusaidia watoto wa kike walioshindwa kumaliza shule katika mfumo rasmi.

Naye Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Gerald Mweri, alisema mradi huo umelenga kuimarisha na kuanzia teknolojia na mawasiliano ikiwamo kuwafundisha walimu na wanafunzi.

Alisema katika mradi huo shule zisizopungua 1,500 za sekondari zitaunganishia 'internet' na kuzipatia vifaa vya TEHAMA kwa kujifunzia pamoja na kuendesha mafunzo ya stadi za kazi pamoja na elimu ya unasihi kwa walimu na wanafunzi.

"Mafanikio yaliyofanywa na serikali kwenye sekta ya elimu ni shule 153 zinafundisha TEHAMA wanafunzi 36,101, kompyuta za mzani 92,667 na projekta 11,132 na ufaulu kidato cha nne ni asilimia 80.65 na kidato cha sita 98.3," alibainisha.

"Elimu bila malipo zimetumika Sh. bilioni 593.9, shule ya mfano ya wenye ulemavu Patandi mkoani Arusha, ukarabati wa shule kongwe 73, ajira za walimu 7,218 na pikipiki kwa maofisa elimu kata na magari kwa maofisa elimu," alifafanua.

Baadhi ya wadau, Mkuu wa Shule ya Sekondari Abdul Jumbe, Rose Semvua, alisema mradi huo utapunguza msongamano darasani na umbali kwa wanafunzi.

"Naona kwenye mradi kuna malengo ya kuongeza vitabu shuleni, ni vyema mradi huu ukaangalia ujenzi wa maktaba shuleni ili vitunzwe vizuri, na pia kuboresha uelewa wa walimu ili kuwa na wanafunzi bora," alisema.

Andrew Mbinde, alisema kuunganisha shule 1,500 kwa TEHAMA ni kazi kubwa na ikifanikiwa ni hatua nzuri kwa nchi, huku akisisitiza kuwa na maandalizi ya kutosha ikiwamo kuhusisha wadau kama REA, TANESCO na kuunganisha shule na vyuo na Mkongo wa Taifa.

Alphoncia Muli, alisema ni vyema wadau wakaeleweshwa namna wananchi watashiriki kwenye uboreshaji wa shule ili kuwe na maandalizi sahihi kuhakikisha miundombinu bora inapatikana.

HABARI KITAIFA




Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu vyombo hivyo kutimiza wajibu wake, kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. Kulia ni Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Wilson Mahera. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NEC yataka wananchi kuheshimu sheria kuelekea uchaguzi mkuu

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema changamoto zinazojitokeza katika uchaguzi ni watu kuingia wakiwa na sheria na kanuni zao bila kuheshimu zilizowekwa na nchi.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu, Semistocles Kaijage, akizungumza katika kikao cha NEC na Wahariri wa vyombo vya habari, jana jijini Dar es Salaam, alisema changamoto hizo zinasababishwa na vyama vya siasa na watu kutokuwa na utayari wa kufuata na kutekeleza sheria za nchi.

"Hakuna uchaguzi katika nchi yoyote unaofanyika bila kufuata Katiba, sheria, maelekezo na maadili," alisisitiza Jaji Kaijage.

Kikao hicho kilikuwa kwa ajili ya maandalizi ya kuelekea Uchaguzi Mkuu, unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28.

Jaji Kaijage alitoa ufafanuzi huo baada ya kutakiwa kueleza Tume imejiandaa vipi kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika uchaguzi uliopita, hazijitokezi katika uchaguzi wa Oktoba.

"Tukisoma vizuri sheria za uchaguzi, maadili ya uchaguzi, Katiba na kuzifuata, matatizo yote haya tusingekuwa tunayapata, kama kila mtu atafuata sheria, kanuni na utaratibu ambazo zimewekwa rasmi," alisema.

Vile vile, alisema watu kutosoma sheria za uchaguzi na sheria za nchi na kujua wapi pa kwenda kutoa malalamiko yao, kunasababisha matatizo hayo kujitokeza.

Alisema kasoro hizo pia zilijitokeza katika uchaguzi mdogo uliopita kwa sababu malalamiko hayakupelekwa kwenye Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi.

Akinukuu kifungu cha 5.11 katika kitabu cha Maadili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020, chini ya kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343, kinachozungumzia Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Kitaifa, Jimbo na Kata katika kutoa adhabu, alisema kamati hizo zinaweza kuchukua hatua kwa kuagiza upande uliokiuka maadili kusahihisha kosa au makosa yaliyotendeka na iwapo italazimu, kuuomba umma msamaha na kutoa onyo au karipio kwa maandishi.

"Utashangaa ukiuliza pengine ni wangapi wamepeleka hoja au malalamiko yao kwenye kamati zinazoundwa chini ya mamlaka haya utakuta hakuna, tunayasaini kuyatekeleza, lakini hatuna utayari wa kuyafuata wala kuyatekeleza," alisema.

Pia alisema katika uchaguzi huu Tume imejielimisha kuhakikisha mitandao yake haitoi mianya ya kuingiliwa na kuchukua tahadhari.

Kuhusu Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuruhusiwa kushiriki upigaji kura wakiwa kwenye nchi wanazoishi, alisema sheria za nchi hazijaweka utaratibu wa kupiga kura ukiwa nje ya nchi.

Alisema wanachoweza kufanya kama wanataka kupiga kura ni kurudi kwenye nchi yao na kushiriki upigaji kura.

Jaji Kaijage, alivitaka vyombo vya habari kutenda haki sawa kwa vyama vyote kwa kuwapa nafasi ya kutangaza na kunadi sera na ilani za vyama vyao.

Pia alisema NEC itaandaa mafunzo kwa waandishi wa habari ambao watahusika na masuala ya uchaguzi ili kuwajengea uwezo.

Naye, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Dk. Wilson Mahera, alisema waandishi watakaoshiriki uchaguzi watasajiliwa na kupewa utambulisho utakaowawezesha kuingia kwenye vituo vya kupigia kura na eneo la kutangazia matokeo.

Pia watandaa chumba chao wakati wa kutangaza matokeo ya uchaguzi wa kiti cha urais ili wafanyie shughuli zao badala ya kwenda ofisini.

# Ununuzi mpunga, mahindi ya wakulima tani 300,000 wiki ijayo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imesema Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), wiki ijayo utaanza awamu ya pili ya ununuzi wa mazao ya nafaka yakiwamo mahindi kutoka kwa wakulima.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Kilito, Japhet Hasunga, jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya uzalishaji mazao ya chakula kwa msimu wa mwaka 2019/2020 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2020/21.

Alisema kwa mwaka 2020/21, NFRA imejipanga kununua tani 300,000 za mahindi, mpunga na mtama.

"Niwahakikishie wakulima wote nchini waliozalisha, mwaka huu NFRA hawanunui tu mahindi, wananunua hadi mpunga, awamu ya kwanza wameshakamilisha kununua na kuanzia wiki ijayo wanaingia awamu ya pili ya kuanza ununuzi," alisema.

"Pia tumeagiza NFRA pamoja na Bodi ya Nafaka Mchanganyiko watafute masoko nje ya nchi ili wakauze kwenye hayo masoko," alisema.

Alifafanua kuwa fedha zilizotumika awamu ya kwanza ni zilizobaki katika mwaka wa fedha 2019/20, na kwamba kilichochelewesha ni utoaji wa fedha serikalini.

"Tumeingia kwenye mwaka mpya wa fedha, hivyo kilichochelewesha kidogo ni upatikanaji wa fedha, tuna imani serikali itatoa fedha hiyo, kati ya wiki hii au ijayo na mambo yatakuwa vizuri," alisema.

Aidha, alisisitiza serikali haitapanga bei ya mazao yoyote, bali itaamuriwa na soko ambapo mzalishaji atapanga bei yake ambayo watakubaliana na mnunuzi.

Akizungumzia hali ya usalama wa chakula, Hasunga alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21 nchi inatarajiwa kuwa na ziada ya tani milioni 3.3 za chakula, ambapo tani milioni 1.32 ni za mazao ya nafaka na tani milioni 2.07 ni za mazao yasiyo nafaka.

"Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2020/21 ni kiasi cha tani milioni 14.3 ambapo mahitaji ya mahindi ni kiasi cha tani milioni 5.7, ikilinganishwa na uzalishaji nchi itakuwa na ziada ya tani 651,314 ambayo ni mara mbili ya ziada iliyopatikana msimu wa 2018/19," alisema.

Pia alisema mahitaji ya mchele ni tani milioni 1.08, kiasi hiki kikilinganishwa na uzalishaji nchi itakuwa na ziada ya tani milioni 1.8.

Hata hivyo, alisema baadhi ya mikoa na halmashauri zimeonyesha kuwa na maeneo yenye dalili za kuwa na upungufu wa chakula nchini, ambapo tathmini imeonyesha mikoa 7 ina dalili zitakazosababisha kuwa na upungufu wa chakula katika halmashauri 12.

Alitaja halmashauri hizo ni Kilwa, Lindi DC, Liwale, Ruangwa, Ikungi, Itigi, Manyoni, Simanjiro, Meatu, Musoma DC na Sumbawanga DC.

Tpb Bank
Grow with us

TPB BANK PLC

TAARIFA KWA UMMA

MPENDWA MTEJA,

TUNAPENDA KUKUTAARIFU KUWA KUTOKANA NA KUUNGANA KWA BENKI YA **TIB CORPORATE NA BENKI YA TPB,** KUTAKUWA NA KUUNGANISHWA KWA MIFUMO YA TEHAMA HIVYO MATUMIZI YA **TIB MOBILE BANKING (*150*45#)** YATASITISHWA KUANZIA TAREHE **28-08-2020.**

TAFADHALI FIKA KATIKA TAWI LOLOTE LA TPB/TIB KUANZIA 31-08-2020 ILI KUUNGANISHWA TENA

Imetolewa Na:
Idara ya Uhusiano na Mawasiliano
Benki ya TPB
0658 767683, 0788 767683 OR 0713 162335

# CHADEMA yaahidi kampeni za kistaarabu

**Na Waandishi Wetu**

**"Arusha Mjini hakuna muujiza kwa vyama vingine tofauti na CHADEMA kushinda uchaguzi ujao. Sisi tutaendelea kushinda ubunge wa jimbo hili na tutaongoza halmashauri kwa kwa kushinda kata zote 25," alisema Lema.**

MGOMBEA ubunge katika Jimbo la Arusha Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Godbless Lema, amesema chama hicho kitahakikisha kampeni zake zinatawaliwa na ustaarabu.

Sambamba na ahadi hiyo, ameiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutenda haki kwa kumtangaza mshindi ambaye atashinda uchaguzi kwa ngazi ya udiwani, ubunge na urais.

Lema aliyasema hayo wakati akichukua fomu ya kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kuwa Mbunge jijini humo.

Alisema chama hicho kimetoa semina kwa wagombea ubunge na udiwani kufanya kampeni za kistaarabu kwa kushindana kwa hoja badala ya kutumia majukwaa ya kampeni kutukana wagombea wa vyama vingine.

Lema ambaye ni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, alisema amechukua fomu ya kugombea kwa kuwa anaamini wananchi wa Arusha watamchagua aendelee kuwa mbunge wa jimbo hilo.

"Arusha Mjini hakuna muujiza kwa vyama vingine tofauti na CHADEMA kushinda uchaguzi ujao. Sisi tutaendelea kushinda ubunge wa jimbo hili na tutaongoza halmashauri kwa kwa kushinda kata zote 25," alisema Lema. Naye mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu, alisema akipata ridhaa ya kuwa rais wa Tanzania, atatoa kipaumbele katika uhuru wa kujieleza na kupata taarifa nchini.

Lissu aliyasema hayo jana wakati akitafuta wadhamini mkoani Iringa na kuahidi kuwa vyombo vya habari vitakuwa kipaumbele chake kuhakikisha wanafanyakazi bila kubugudhiwa.

"Leo ukiangalia vyombo vya habari vya ndani ya nchi vinafanya kazi ila havifanyi kazi yake kwa uhuru, jambo ambalo kwenye serikali yangu waandishi wataishi vizuri na kufanya kazi zao kwa uhuru zaidi siyo Watanzania waishi kwa kutegemea kupata habari kupitia makundi sogezi na mitandao mingine ya kijamii," alisema.

Lissu alisema kipaumbele kingine ni kuwalinda wafanyabiashara na kuhakikisha tozo halali za kodi zinazotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na kitakuwa chombo cha kutoa haki kwa mlipa kodi.

Aidha, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kuenzi demokrasia ya vyama vingi bila kunyanyasa raia wala vyama na kwamba tangu wamefika mkoani humo na mkoa wa Morogoro wamepata ushirikiano wa kutosha.

Kwa mujibu wa Lissu, Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu utakuwa huru na haki kwa vyama vyote kunadi sera zake bila kunyanyasika na wao kama CHADEMA hawatakuwa tayari kuona amani ya nchi inavurugwa.



Mgombea urais wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu (kulia), akiwa na mgombea ubunge Jimbo la Iringa Mjini, Mch. Peter Msigwa, walipofanya mkutano wa hadhara katika viwanja vya Mwembetogwa, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mtiania wa udiwani CCM atimkia CUF

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

MTIANIA ya udiwani kwenye mchakato wa kura za maoni wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Mkuti Halmashauri ya Mji wa Masasi, Roger Mbotela, amekihama chama hicho na kujiunga na CUF na juzi alichukua fomu ya kugombea nafasi hiyo.

Mbotela katika mchakato wa kura za maoni ndani ya CCM alipata kura 11, huku aliyeongoza akipata kura zaidi ya 100.

Alidai amechukua uamuzi huo kutokana na kustaajabishwa na matokeo hayo, na kwamba hakutarajia kushindwa kwa kupata kura chache.

Akizungumza na waandishi wa habari wilayani Masasi baada ya kutangaza uamuzi wa kujiunga na CUF, Mbotela alisema uamuzi huo umekuja baada ya kupata kura chache.

Aliongeza kuwa kura alizopata hakuzitarajia, hivyo matokeo hayo yamemsukuma kuhamia CUF ambayo imempatia ridhaa ya kugombea nafasi hiyo baada ya kukabidhiwa kadi ya uanachama.

"Nimetumia haki yangu ya kikatiba kuhama CCM na kujiunga CUF, ninachohitaji ni mabadiliko, kwa kuwa nimeangushwa kwenye kura za maoni katika Chama Cha Mapinduzi, basi nitayapata mabadiliko hayo ndani ya CUF, ndio maana nimekuja huku kwani hakuna mtu anayezuiliwa kuhama chama na kujiunga na kingine," alisema Mbotela.

Mwenyekiti wa CUF Wilaya ya Masasi, Yusuph Matola, alithibitisha kumpokea mwanachama huyo mpya na wameshamkabidhi kadi, lakini pia wamempa ridhaa ya kugombea udiwani Kata ya Mkuti.

Katibu wa CCM Wilaya ya Masasi, Shaibu Mtawa, alipoulizwa kuhusu mwanachama huyo kuhamia CUF, alisema amesikia na kuona katika mitandao ya kijamii, hivyo kwake sio jambo ngeni mwanachama kuhama CCM na kwenda chama kingine.

**"Nimetumia haki yangu ya kikatiba kuhama CCM na kujiunga CUF, ninachohitaji ni mabadiliko, kwa kuwa nimeangushwa kwenye kura za maoni katika Chama Cha Mapinduzi, basi nitayapata mabadiliko hayo ndani ya CUF...**

# Zitto: Mpango vyama kushirikiana bado upo

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimesema mpango wa vyama vya upinzani kushirikiana katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu bado upo licha ya kuwa kila chama kwa sasa kimeshateua wagombea wake kwa nafasi za udiwani, ubunge na urais.

Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa mazungumzo baina ya vyama vya upinzani bado yanaendelea kwa lengo la kuhakikisha panakuwapo ushirikiano katika uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

"Mkutano Mkuu wa chama chetu uliridhia azimio la baraza kuu kwamba tuhakikishe tunapambana pawapo na ushirikiano wa vyama makini vya upinzani mpaka dakika ya mwisho na sisi tunaendelea kuhakikisha hilo.

"Mazungumzo yanaendelea na ndugu Bashange ni mmoja wa viongozi wetu wanaoshiriki kwenye mazungumzo hayo na Makamu Mwenyekiti wa Chama Taifa, Dorothy Semu, ndiyo viongozi wa jopo la mazungumzo kutoka ACT-Wazalendo na ninaamini tutakuwa na ushirikiano wa vyama, sina shaka na hilo hata kidogo," Zitto alisema.

Katika mkutano huo na waandishi wa habari, Zitto pia alilalamika kuhusu kile alichodai kupigwa kwa wagombea wao wa ubunge katika Mkoa wa Lindi, akilitaka Jeshi la Polisi kufuatilia suala hilo, ili kuhakikisha panakuwa na amani na utulivu nchini.

Wanachama hao wanaodaiwa kupigwa ni Joackim Ng'ombo, mkazi wa Kijiji cha Nangumbu wilayani Ruangwa mkoani Lindi na Said Nangendekwa kutoka wilaya hiyo hiyo ambaye anadaiwa kuumizwa sehemu mbalimbali za mwili wake na watu wasiojulikana.

"Tumewauliza Jeshi la Polisi, wametuambia bado wanaendelea na upelelezi, tunaomba na tunamtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi, ndugu (Simon) Sirro, afanye haraka upelelezi wa matukio haya ukamilike kwa sababu hatutaki uchaguzi ambao una damu," Zitto alisema.

Katika hatua nyingine, kiongozi huyo amewatambulisha wasimamizi wa kampeni za chama hicho katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu ambao ni Joram Bashange, Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Tanzania Bara, ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kampeni na Emmanuel Mvula atakayekuwa Meneja Kampeni wa chama hicho.

HABARI KITAIFA

# Waandamana kisa 'kukatwa' walioongoza kura za maoni

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

BAADHI ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamekusanyika ofisi za chama hicho Wilaya ya Dodoma mjini wakilalamikia kuenguliwa kwa wagombea wa udiwani walioongoza kwenye mchakato wa kura za maoni.

Wakizungumza nje ya ofisi hizo jana, baadhi ya wananchi hao kutoka Kata za Makutupora, Chang'ombe na Ipagala na Kikombo, walidai walifika ofisini huko kwa lengo la kuujulisha uongozi wa CCM wilaya kuwa hawajakubaliana na uamuzi wa kuwaengua wagombea waliowachagua.

Mkazi wa Kata ya Chang'ombe, Athumani Ally, alisema kuwa juzi walitajiwa jina la Juma Ikaba kuwa ameteuliwa kugombea udiwani katika kata hiyo, lakini jana asubuhi wakajulishwa kuwa Bakari Juma ndiye ameteuliwa kupeperusha bendera ya chama hicho katika kata hiyo.

"Sasa utata huu hatuwezi kuendelea kuvumilia Chang'ombe, tumeona tufike ofisi za chama Wilaya ili kupata majibu ya uhakika maana huu ni ubabaishaji wa hali ya juu, hatukubali," alisema.

Aliyekuwa mgombea udiwani kupitia chama hicho katika kata hiyo, Ikaba, alisema wananchi waliofika ofisini huko ni sehemu ya wengi waliobaki huko Chang'ombe.

Ikaba alisema wamefika ofisi za chama ili kupata uhakika wa jina lililoteuliwa na chama hicho kugombea udiwani kwa kata yao.

"Hapa hatujaja kufanya fujo, tumefika na kupokewa vizuri na uongozi wa CCM wilaya na wametuambia turudi nyumbani na majibu yatakuja kutolewa huko kwenye ofisi zetu," alisema.

Wananchi wengine waliofika kwenye ofisi hizo walidai kutoka kata za Mkonze, Mkutupora, Ipagala, Kikombo, Nkuhungu, Kikombo na Chang'ombe na wengi walikuwa na malalamiko kuhusu uteuzi wa wagombea wa nafasi za udiwani, wakihoji sababu za kuenguliwa kwa makada walioongoza kura za maoni. Mkuu wa Polisi Wilaya ya Dodoma, Kidward Karinga, akizungumza na wananchi hao ofisini huko jana, aliwataka kuondoka eneo hilo kwa sababu za kiusalama.

Alionya kuwa yeyote kwa kukiuka agizo hilo, hatua za kisheria zingechukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani kwa kufanya kosa la jinai.

Karinga aliwataka wananchi hao kufuata taratibu za kuwasilisha malalamiko yao na kuepuka kufanya maandamano ambayo yanaweza kuhatarisha usalama wa raia wema.

Baada ya kutolewa kwa amri hiyo ya Jeshi la Polisi wafuasi hao wa makada wa CCM waliondoka kwenye ofisi hizo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma, Elirehema Nassari, alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, alisema hawezi kulizungumzia na kuwaomba wafuasi hao kusubiri uamuzi wa vikao vya juu vya chama hicho.

Nipashe pia ilimtafuta Kaimu Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma, Pili Mbaga, ambaye pia alisema hawezi kuzungumza kwa madai kuwa alikuwa kwenye kikao.



Katibu wa Shirika linalojishughulisha na kutetea haki za wanawake na watoto la YWCA Tanzania, mkoani Shinyanga, Marysiana Makundi, akizungumza jana, wakati akitambulisha mradi wa mwaka mmoja wa wazazi kuwajibika kwa watoto wao, utakaotekelezwa kwenye Kata ya Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mgombea urais UPDP: Walarushwa kwenda jela miaka 100, viboko 100

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha UPDP, Twalib Ibrahim Kadege, amesema kama wananchi watakipa ridhaa chama hicho, kitatunga sheria kali kwa wala rushwa ambapo watakuwa wanachapwa viboko 100 hadharani na kifungo cha miaka 100 jela.

Akizungumza katika mahojiano maaluma na gazeti hili jana, alisema rushwa imekuwa tatizo sana katika nchi hii ingawa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk John Magufuli imejitahidi kudhibiti kwa kiwango cha asilimia 60 tu.

"Rais wa sasa John Magufuli amefanikiwa kupambana na rushwa, sisi tutatunga sheria kali za kuwadhibiti wala rushwa na wale waliohujumu uchumi wetu," alisema.

Kadege alisema sheria iliyopo sasa ya kupamba na rushwa haijitoshelezi ndo maana watu wanaendelea na vitendo vya rushwa kwa kuwa wanajua hata wakibainika wametenda kosa hilo hawatafungwa zaidi ya miaka 30.

"Kuna nchi kama China ni vigumu mtu kula rushwa sababu sheria yao ni kali ambayo ukibainika adhabu yake ni kupigwa risasi,..na sisi itabidi kuweka sheria kali," alisema.

Kadege alisema sera ya kulindana ndio imeifikisha Tanzania kuwa katika hali mbaya kiuchumi kabla Magufuli hajaingia madarakani kwa sababu ya sera za kulindana.

"Tunashukuru Rais Magufuli alipofika ameondoa kulindana, mtu akiharibu mtu anafukuzwa, na anapelekwa mahakamani, sisi tukiingia madarakani tutamfunga mtuhumiwa wa rushwa miaka 100 asitoke, afie jela kabisa," alisema.

Kadege aliongeza kuwa mambo mengine ambayo serikali ya chama hicho itayafanya iwapo watapata ridhaa ya wananchi, ni kuboresha mishahara ya wafanyakazi ambapo kiwango cha chini cha mshahara kitafikia Sh. 500,000.

Alisema wananchi wasiokuwa na ajira watakuwa wanalipwa Sh. 200,000 kila mwezi kwa lengo la kupunguza ukali wa maisha.

"Nchi yetu ni tajiri sio maskini, haya yote yanawezekana, cha msingi ni kuziba mianya ya rushwa kwani rushwa ni adui wa haki, rushwa ndio inadumaza maendeleo, inadumaza uchumi, inadumaza afya, inadumaza kila sekta katika nchi," alisema.

Kuhusu kampeni, alisema chama chake kimejipanga kuhakikisha wanafika katika mikoa yote nchini, na kwamba fedha wanazotegemea ziwasaidie ni michango ya wanachama na wananchi.

## Chuo chapania kupunguza uhaba wataalamu wa afya

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Kumbukumbu ya Profesa Hubert Kairuki (HKMU), kimepanga kujipanua zaidi ikiwa ni jitihada za kuzalisha watumishi wa kada mbalimbali ili kupunguza uhaba wa watumishi kwenye sekta ya afya.

Hayo yalisemwa jana na Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Charles Mgone, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu mikakati ya chuo hicho kuongeza udahili na kuzalisha madaktari na wakunga wengi.

Prof. Mgone alisema chuo hicho kitajitahidi kwenda na wakati kwa kuhakikisha taaluma inazingatiwa katika kutoa madaktari na watumishi wengine wa kada ya afya.

"Sisi tuliona mbele kabisa kwamba katika sehemu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) tunaitumia kama msingi wa mafunzo ya vitendo tunataka kila kitu kiwe kwenye elektroniki badala ya kutembea na makaratasi," alisema.

Alisema walishafanya tathmini ya uhalibifu wa mazingira kwa ajili ya kujenga kampasi hiyo na matayarisho yatakapokamilika wataanza ujenzi kidogo kidogo kulingana na fedha zilizopo.

Kwa mujibu wa Prof. Mgone, chuo kimeomba fedha kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa kampasi hiyo maeneo ya Boko ambako ni nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Alisema uwiano wa daktari mmoja na mgonjwa kwa Afrika ni mkubwa sana na ndoto ya mwanzilishi wa chuo hicho, Prof. Hubert Kairuki, ilikuwa kupunguza tatizo hilo kwa kiwango kikubwa nchini.

Chuo hicho, alisema licha ya kutoa madaktari wa shahada ya kwanza, pia kimekuwa kikifundisha na kuzalisha madaktari bingwa kwenye fani ya tiba.

Pia alisema kwa wastani kwa mwaka wamekuwa wakizalisha zaidi ya madaktari 200 na wanatarajia idadi hiyo itaongezeka kutokana na upanuzi wa chuo hicho unaotarajiwa kufanywa.

Alisema ili malengo ya Umoja wa Mataifa yaweze kufikiwa lazima mambo mengi yafanyike ikiwamo kutoa mafunzo mahiri kwa wahudumu wa sekta ya afya.

Wakati wa Uhuru, alisema wastani wa daktari mmoja kwa mgonjwa ilikuwa 1: 25,000 na kwa sasa daktari mmoja anahudumia watu 20,000 jambo ambalo bado si la kujivunia.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabinti wasiachiwe kuumizwa na maradhi

SERIKALI imeendeleza juhudi za kuwasomesha watoto kuanzia shule za msingi hadi sekondari ili kuwaondoa kwenye umaskini, ujinga na maradhi, ambayo ni maadui wakuu wa taifa.

Lakini pamoja na jitihada hizo inasikitisha tena kusikia kuwa wasichana wenye umri wa miaka kati ya 16 na 24 ambao walitakiwa kuwa shuleni iwe sekondari, vyuo vikuu au vya kati, wananaswa tena kwenye mtego wa kuambukizwa UKIMWI.

Taarifa hizo zinazotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) Leonard Maboko, kuwa wasichana wanaambukizwa magonjwa kwa sababu ya kukosa jinsi ya kujiongezea kipato.

Anasema kuwa asilimia 40 ya maambukizi mapya ya VVU idadi kubwa inapatikana kwa wasichana ambao ndiyo wazazi na walezi wa taifa na ambao wako katika umri wa uzazi.

Hiyo ni changamoto na kila mmoja mwenye nia njema kwa watoto na vijana wa Tanzania ambao wanatakiwa kuwa na elimu, ulio ufunguo wa maisha anaguswa na namna ambavyo VVU inaweza kuwa chanzo ya kuvuruga maisha ya vijana wasichana.

Tunaipongeza serikali kwa kujitahidi kuwapima na kuwapa dawa na ushauri wanaoonekana kuwa na maambukizi kupitia kampeni ya Furaha Yangu, lakini nia hii njema inakwamishwa na kasi kubwa ya mabinti kuambukizwa VVU.

Pamoja na mkakati huo tungependa kuishauri serikali kuwa kuna haja ya kuwatizama wasichana hawa kwa jitihada zaidi ili kudhibiti maambukizi hayo.

Wanahitaji kusoma na kumudu maisha yao si kuambukizwa maradhi njia mojawapo ikitajwa kuwa ni kwa sababu wanakosa kipato.

Tunaona kuwa ni vyema kuhamasisha zaidi wadau na jamii kulivalia njuga suala hili ambalo linawaumiza wasichana na hata taifa ambao badala ya kuingia darasa na kujifunza masuala ya taaluma ili kuendeleza maisha yao na ya vizazi vyao, wanaanza kuwa waathirika wa magonjwa wanayoyapata kwa kiasi kikubwa kutokana na kunyanyaswa kijinsia na kingono.

Kama ambavyo serikali imeanza kuhimiza wanafunzi wasome ni vyema pia mabinti hawa walindwe ili wasome na kusaidiwa kwa hali na mali ili kuwaepusha na maambukizi, mimba na ndoa za utotoni na kuhakikisha kuwa wananufaika na mafunzo mbalimbali na taaluma rasmi zinazotolewa vyuoni na shule kwa vijana wenye umri wao.

Pamoja na kuwaibua wasichana hao kuwa wanaishi na VVU ni muhimu wasaidiwe kitaaluma na kushauriana na wazazi na walezi wao ili kuona namna bora ya kuwasaidia kwani wengi hawezi kuendelea kwenye shule na vyuo vikuu baada ya kufahamu kuwa wameathirika na maradhi.

Hapo ndipo tunapoishauri serikali kuona uwezekano wa kuwa na vyuo vya ufundi maalumu na taaluma mbalimbali kwa ajili ya kusaidia makundi mbalimbali ya watu wanaoishi na matatizo ili badala ya kujiingiza kwenye uhusiano wawe na stadi mbalimbali za kujiajiri na kupata kipato.

Vyuo hivyo vinaweza kuanzishwa baada ya kuwatambua watu hao wenye mahitaji maalumu ya aina mbalimbali wanaoishi kwenye jamii mijini na vijijini.


Ni hatua nzuri ya kuwasaidia kupata elimu japo wapo ambao hawako tayari kusoma hivyo wakati mwingine ni kuwafuatilia na kuwasikiliza ili kukijua kile ambacho wanakihitaji.

Wapo wanaopenda kuendelezwa kwa stadi mbalimbali za kiuchumi, wengine kiufundi, wapo pia wanaohitaji mitaji au vifaa vya kazi kama mashine au mifugo.

Ni rai yetu kuwa pamoja na serikali kuwasaidia, siku za usoni ifanye utafiti wa kuona jinsi utoaji wa elimu ulivyoweza kuzisaidia familia zenye watu wanaoishi na changamoto za umaskini ili kuibua mikakati mipya na bora zaidi ya kuwaondoa kwenye changamoto zikiwamo kuanzisha uhusiano wa kingono katika umri mdogo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Uchaguzi huu vijana wasiwe mbeleko kubeba wanasiasa

MOJA ya mahitaji ya vijana katika siasa ni kuwa na uwakilishi kwenye vyombo vya maamuzi na kuwakilishwa kikamilifu bungeni na kwenye majukwaa muhimu yanayohusika na maendeleo ya taifa. Mahitaji yao hayo yamefanyiwa kazi na sasa wanachaguliwa katika nafasi mbalimbali zikiwamo za ubunge na udiwani, ili kuwawakilisha kwenye vyombo vya maamuzi.

Pamoja na mafanikio hayo, ni vyema wakatambua kuwa mahitaji yao yote hayawezi kutimizwa iwapo hawashiriki kikamilifu kwenye mchakato wa kisiasa na kujikuta wakitumika kwa manufaa ya wanasiasa wachache.

Vijana wanatakiwa kuomba ridhaa ya uwakilishi, katika ngazi mbalimbali kuanzia kwenye udiwani hadi ubunge badala ya kuwa madaraja ya kufanikisha ajenda za baadhi ya wanasiasa.

Ikumbukwe kwamba, ni kundi linalotarajiwa kuwa na idadi kubwa ya wapigakura na viongozi wa baadaye wa vyama vya siasa na serikali kwa ujumla na pia wanatajwa kama taifa la kesho na nguvukazi muhimu.

Lakini bahati mbaya, baadhi yao wamekuwa wakitumiwa na wanasiasa kama madaraja ya kuwavusha kufika malengo yao licha ya kuwaacha bila mafanikio na wakati mwingine katika kutetea maslahi ya wanasiasa hao, vijana hujikuta wakiumizana wenyewe kwa wenyewe, ili mradi tu watimize kile ambacho wameambiwa kukifanya hata kama kitakuwa ni hatia.

Kutokana na mazingira kama hayo, ambayo yanajitokeza wakati wa uchaguzi, ni vyema sasa vijana wakajitambua na kuepuka kuwa mbeleko za kuvusha wanasiasa wasio na mpango wa kuwaendeleza.

Ni vyema kujihadhari wasiteswe na ushabiki wa kisiasa bali waandaliwe vyema, ili kuwa raia na wazalendo wema na pia wanaowajibika, kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya nchi yao badala ya kuwanufaisha watu wachache. Huu ni mwaka wa uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani, hivyo ni vyema kukumbuka masuala muhimu ya kiuchaguzi.

Kwa sasa kuna mchakato unaendelea kabla ya kampeni za uchaguzi huo, ambazo zitaanza Agosti 26 mwaka huu, hivyo si vibaya kutoa angalizo kwa vijana kuwa makini ili wasitumike kama madaraja ya kuvusha wanasiasa.

Imekuwa ni kawaida kila mwaka uchaguzi, vijana ndiyo hutumiwa na wanasiasa kufanikisha kile wanachokitaka, hivyo wasikubali kutumika kufanya mambo ambayo hayafai na kujikuta wakihasimiana wenyewe kwa wenyewe.

Katika uwanja mpya wa demokrasia duniani, vijana wanatakiwa kupewa kipaumbele na umuhimu wa kipekee kwa kuwa ni viongozi watarajiwa wa baadaye, hivyo wanapaswa kuandaliwa vyema.

Wakiwa wameandaliwa vyema hawatakuwa tayari kukubali kutumiwa na wanasiasa kuvuruga amani, usalama na uelewano wa kijamii, bali watazingatia ustawi, maendeleo na manufaa ya Watanzania.

Vijana wanatakiwa kuwa makini, itikadi za vyama vya siasa zisiwagawe bali watambue kuwa, wao ndiyo nguvukazi ya taifa na taifa la kesho wanaotakiwa kuandaliwa vizuri na siyo kutumiwa kwa manufaa ya wachache.

Taifa hili lina hazina kubwa ya vijana wanaoishi mijini na vijijini, ambao wanatakiwa kuandaliwa kuliongoza, siyo kuvusha wanasiasa ama kuwagombanisha.

Kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya mwaka 2012 asilimia 77 ya watu wa Tanzania, wana umri ulio chini ya miaka 35, na asilimia 19 wana umri kati ya miaka 15 hadi 24, ambao wote kwa ujumla ni vijana.

Hivyo wakati nchi inaelekea katika uchaguzi mkuu, vijana hao wasikubali kutumiwa na wanasiasa kufanya vurugu badala yake watambue kuwa wana haki ya kushiriki katika uchaguzi huo kwa amani na utulivu.

Wakati umefika kwa vijana kujitambua na kujiongeza wakikataa kutumika kisiasa kwa ajili ya maslahi binafsi au kujijenga kisiasa, badala yake wanatakiwa kujiangalia maisha yao na kuona mbali na siyo kukubali kutumiwa kisiasa kama ambavyo baadhi yao wamekuwa wakifanya na kuwa chanzo cha vurumai na vurugu.

# BURIANI HASSAN NASSOR MOYO

- *Mwasisi ASP, CCM, Mapinduzi, Muungano*
- *Mratibu Maridhiano Zanzibar CCM, CUF*
- *Umati wamzika; Karume, Mwinyi, Jussa*

**Na Waandishi Wetu, DAR, UNGUJA**

NI mtikisiko katika historia ya siasa nchini katika Jamhuri ya Muungano, Mzee Hassan Nassor Moyo (pichani), mwasisi wa mengi ya kihistoria nchini amefariki dunia alfajiri ya jana, nyumbani kwake mkoani Tanga. Hadi asubuhi jana taarifa zilishasambaa kila mahali kimataifa.

Umekuwa msiba mkubwa wa Watanzania wote, kwanini mwanasiasa aliyebeba ishara kuu zisizopungua tano zinazobaki kuwa historia ndani ya Tanzania.

Mzee Moyo, mzaliwa wa Septemba 27, mwaka 1933 alifariki akiwa na umri wa miaka 87 na kuzikwa jana, Unguja, kutokana na wosia aliyoacha.

"Wakati wa uhai wake Mzee Moyo alisema kuwa atapofariki dunia, azikwe katika makaburi aliyozikwa mama yake eneo la Fuoni, karibu na nyumba yake," anasema Mohamed, mtoto wa marehemu.



Kwa mujibu wa mtoto huyo wa marehemu, baba yake alihamia mkoani Tanga miaka miwili iliyopita alikokuwa na makazi yake, alizikwa jana Unguja kutokana na wosia aliyoacha.

Historia na mzizi wa maisha ya Mzee Moyo, unabeba mengi ya misingi kiserikali, kichama na kisiasa ndani ya Jamhuri ya Muungano yanayobaki kuwa alama.

Mojawapo, alishapata wajibu wa kusimamia na kushiriki uamuzi nyeti katika maeneo hayo, yanayobaki kuwa tafsiri ya kudumu nchini, katika mustakabali wa rekodi ya siasa za kimataifa.

Visiwani Zanzibar, kunapozungumziwa kuasisiwa Chama cha Afro Shirazi (ASP), Februari 5 mwaka 1957, Mzee Moyo alikuwa miongoni mwa waliofanya kazi hiyo.

Pale, chama hicho kilipojiunga na wenzao wa TANU upande wa pili wa Tanzania Bara kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM), Februari 5, 1977, pia anapatikana katika orodha ya waasisi, akiwa na kadi Namba Saba.

Inaporejewa kiserikali na siasa za mwaka 1964 visiwani, Mzee Moyo anatajwa kushiriki Mapinduzi ya Zanzibar yaliyoiondoa serikali ya kisultani, vivyo hivyo mwaka huohuo katika tukio la muungano.

Ilikuwa Aprili, 1964, alijitokeza tena kati ya waasisi kutoka Zanzibar walioshiriki kubadilishana hati za kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwasisi huyo anatajwa katika orodha ya wajumbe saba wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, walioapishwa kuwa wabunge Jamhuri ya Muungano, baada ya kushiriki tendo la kubadilishana hati zinazohusika.

Wengine wanatajwa ni Sheikh Abeid Amani Karume, Aboud Jumbe Mwinyi, Sheikh Idris Abdul Wakil (wote walioshika nafasi ya urais Zanzibar katika vipindi tofauti), Kassim Abdallah Hanga, Abdulrahaman Mohamed Babu na Hasnu Makame .

Baada ya kuapishwa kuwa wabunge, Moyo na wenzake hao waliteuliwa kuwa mawaziri katika Serikali ya Muungano akiwa na historia ndefu ya kutumikia nafasi hizo, Zanzibar na Bara. Katika zama za mwisho, aliongoza wizara nyeti ndani ya Muungano.

Ndani ya kipindi cha Tanzania yenye siasa ya vyama vingi kuanzia mwaka 1992, Visiwani Zanzibar kulikumbwa na baadhi ya sintofahamu za kisiasa, ikiwamo tukio la kihistoria la mauaji ya Pemba, 1991.

Mnamo Novemba, 2009, kuliundwa Kamati ya Maridhiano Zanzibar, na Mzee Moyo alipewa jukumu la kuratibu namna ya kuzikutanisha pande zinazotofautiana kisiasa, lengo ni kusafisha na kujenga wigo uliojaa sura ya amani Zanzibar.

Wajumbe wengine katika kamati hiyo ni Mansour Yussuf Himid, Mohammed Riyami, Abubakar Khamis, Ismail Jussa na Salum Bimani.

Kupitia kamati hiyo, iliwakutanisha baadhi ya wahusika muhimu kama, Rais Mstaafu wa Zanzibar (awamu ya sita), Dk. Aman Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa mgombea urais na Katibu Mkuu wa Chama Kikuu cha Upinzani, Civic United Front (CUF), ambao pia ndio watajawa kuasisi wazo hilo.

Maalim Seif, kwa sasa ni Mwenyekiti wa Chama cha ACT - Wazalendo na mgombea urais wa Zanzibar katika uchaguzi mkuu ujao, akiwa na historia ya kutumikia nafasi ya Waziri Kiongozi, katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Kamati ya Mzee Moyo, ilipewa jukumu kuratibu na kutafuta mbinu za kuondoa tofauti za kisiasa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2010, hatima yake iliundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, baada ya kufanyika marekebisho ya Katiba ya SMZ.

Baada ya kufanyika uchaguzi wa Zanzibar 2010, iliundwa 'Serikali ya Pamoja' iliyoongozwa na Rais Dk. Ali Mohammed Shein, akisaidiwa na Makamu wa Kwanza, Maalim Seif aliyesaidiwa na Makamu wa Pili, Balozi Seif Ali Iddi.

Hiyo ilikuwa katika miaka mitano ya kwanza ya uongozi wa Rais Dk. Shein, anayekamilisha sasa vipindi viwili vya uongozi, jumla miaka 10.

Jukumu la Kamati ya Maridhiano iliyoundwa, halikufikiwa mwisho, baada ya mdau muhimu, Maalim Seif kujitoa, kwa madai ya kutokukubalina na baadhi ya mambo katika mwenendo wa maridhiano hayo.

Baadaye mwaka 2015, Mzee Moyo baada ya kukumbwa na misukosuko ya kisiasa ndani ya chama chake- CCM alivuliwa uanachama, kupitia iliyofikiwa na kikao cha chama, Mkoa wa Magharibi, Unguja.

Katika uwasilisho wa wasifu wake jana mazikoni, maisha yake yote Mzee Moyo anatajwa alihubiri amani, akitaka kuwa msimamo wa Wazanzibari kila mahali.

**MAZIKONI**

Majira ya jioni jana, umati mkubwa ulijitokeza katika makaburi ya Fuoni, kukihudhuriwa pia na viongozi mbalimbali wa SMZ, akiwamo Rais mstaafu, Amani Abeid Karume, anayetamka aliheshimu sana hekima na busara zake marehemu.

Pia, walikuwapo mawaziri na wanasiasa mbalimbali wa Zanzibar, akiwamo mgombea urais-CCM, Dk. Hussein Mwinyi, aliyetamka: "Alikuwa mwasisi mkubwa wa taifa hili, kwa hiyo msiba huu umetushtua sana."

Ismali Jussa, aliyekuwa Mjumbe Mwenza wa Kamati ya Maridhiano, alieleza kumuenzi Mzee Moyo kwa misimamo aliyochukua katika Kamati ya Maridhiano kupigania umoja na mshikamano katika Katiba mpya ya Zanzibar na anamtaja alikuwa muumini wa mamlaka ya Wazanzibari.

# Zaipuna bosi mpya wa NMB

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Wakurugenzi ya Benki ya NMB imemtangaza Ruth Zaipuna kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu (CEO) wa benki hiyo. Uteuzi ulianza jana.

Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede, alimtangaza Zaipuna huku akikiri kuwa mchakato wa kumpata haukuwa mwepesi, lakini hakukuwa na upendeleo isipokuwa walitazama wasifu, utendaji na maslahi ya benki na Tanzania.

Alisema katika kipindi kirefu benki hiyo ilikosa mtu baada ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wake kuondoka, hivyo walibaki na mtu aliyekuwa anakaimu kwa zaidi ya mwaka mmoja na nusu, lakini takwa la kisheria lilikuwa linawabana kuwa ni lazima wapate mtu.

Zaipuna anakuwa Mtanzania wa kwanza kushika nafasi hiyo tangu benki hiyo ilipobinafsishwa ambapo kwa nyakati zote nafasi za juu zilishikwa na wageni wakiwamo Ineke Bussemaker aliyekuwa Mkurugenzi tangu 2014 – 2018 kisha nafasi hiyo ikachukuliwa na Albert Jonkergow ambaye alishikiria kwa kipindi cha mpito cha miezi sita kabla ya Zaipuna kupewa nafasi ya kukaimu.

Mwenyekiti alisema mchakato wa kumpata Mtendaji Mkuu ulikamilika Juni 30, 2020 na jana ilikuwa ni siku ya kumtangaza, huku akibainisha kuwa sifa zote zilizotakiwa katika nafasi hiyo, walijiridhisha kuwa Zaipuna anazo, hivyo hakuna shaka kuhusu utumishi wake katika nafasi hiyo.

"Katika kipindi chote tulihangaika kumpata mtu mwenye kufikia vigezo vinavyotakiwa, lakini wakati mwanamama huyu alipokuwa anakaimu, benki imeendelea kufanya vizuri zaidi na kukuza mtaji wake, hakuna mahali paliyumba chini ya usimamizi wake, hivi kwa hali hiyo mnadhani tungefanyaje,' 'alisema Dk. Mhede.

Alitaja mafanikio makubwa katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu wa kukaimu kwa ofisa huyo ni faida kubwa ambayo benki imekuwa ikipata ikiwamo Sh. bilioni 93 zilizopatikana katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2020, huku mahusiano yakizidi kuimarika kati ya benki na serikali pamoja na wateja wake.

Hata hivyo, alimuagiza mtendaji huyo kuhakikisha benki inaendelea kuwa imara na yenye kutoa matumaini kwa wananchi wake, huku akisisitiza ushirikiano wa timu moja kati ya kiongozi huyo na watumishi wengine ndani ya taasisi yao.

Akizungumza baada ya kupokea uteuzi huyo, Zaipuna alisema ni uteuzi wa ushindi kwa NMB wala siyo yeye, lakini akaahidi kwamba atakuwa mtumishi kama ilivyo kwa watumishi wengine.

Alitaja vipaumbele vitano atakavyoanza navyo ikiwamo NMB kuendelea kukua kila mwaka na kuwa benki namba moja nchini, benki kuendelea kuwa chaguo la wateja, kuongeza na kuimarisha mashirikiano kwa wateja na watumishi na kipaumbele cha tano ni kuendelea kuboresha maslahi kwa watumishi ili vijana wa Kitanzania wavutiwe na kutamani zaidi waajiriwe NMB.

Alisema hayo yote yatawezekana ikiwa kila mtumishi atakuwa na nidhamu ya utekelezaji na kujituma.

Kuhusu wanahisa, aliitaja Serikali ya Tanzania na wabia wa benki ya Rabo ya Uholanzi kwamba waondoe hofu kuhusu NMB kwani ni chombo kilichosimama kwa ajili ya kutoa matumaini kwa watu hivyo wataendeleza kasi hiyo wakati wote.

Awali Mjumbe wa Bodi, Margaret Ikongo, aliwataka wajumbe kutoa ushirikiano mkubwa kwa CEO wao mpya kwa kuwa kazi anayokwenda kuifanya ni kubwa na ndiye mbeba maono wa chombo hicho hivyo ushindi wake utategemea nguvu ya pamoja na watumishi ikiwamo kumwombea.




Ofisa Mkuu Msimamizi wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Julius Mjenga (kulia), akimpa elimu ya kodi mfanyabiashara wa eneo la SIDO, mkoani Kigoma jana, kuhusu umuhimu wa utoaji risiti za kodi za kielektroniki wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMISEMI yaziagiza h/shauri ujenzi miradi

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imeziagiza halmashauri zote nchini, kuanza maandalizi ya ujenzi wa miradi ya maendeleo inapoainishwa ili kurahisisha utekelezaji wake fedha zinapotolewa na Serikali.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Joseph Nyamhanga, ndiye aliyetoa agizo hilo juzi akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Jiji la Dar es Salaam.

Alisema amekutana na changamoto za fedha kusubiri maandalizi ya utekelezaji wa miradi, badala ya utekelezaji kusubiri fedha, hali inayozidi kuchelewesha miradi ya maendeleo.

"Nitoe maagizo kwa halmashauri zote nchini, kuhakikisha wanaanza maandalizi ya utekelezaji wakati wakisubiri fedha kutoka serikalini badala ya kukaa mpaka fedha zitoke na matokeo yake ndio nakutana na miradi haijaanza wakati fedha zishatoka," alisema Nyamhanga.

Akikaguza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni, Nyamhanga, alitumia fursa hiyo pia kuziagiza halmashauri zinazojenga wodi tatu katika hospitali 67 za awali nchini, kuanza maandalizi kujenga ili fedha zinapotolewa waanze utekelezaji mara moja.

"Niagize nchi nzima, tuna mpango wa kujenga wodi tatu tatu katika hospitali za wilaya 67 sawa na wodi 201, hivyo nitoe maagizo kwa wakurugenzi wa halmashauri hizo ambazo zimetengewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, kufanya maandalizi mapema," alisema Nyamhanga.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sophia Msafiri, aliishukuru Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kujenga Hospitali ya wilaya hiyo, ambayo kwa kiasi kikubwa itapunguza adha wanazopata wagonjwa.

Alisema wagonjwa wamekuwa wakilazimika kusafiri umbali mrefu kwenda wilayani Temeke kupatiwa matibabu kutokana na kutokuwapo kwa hospitali yao.

Kadhalika, Nyamhanga alitembelea ujenzi wa madarasa 20 na matundu vya vyoo 10 katika Shule ya Msingi Mbagala yenye wanafunzi 2,848 na kuagiza ujenzi ukamilike kwa wakati.

Pia, alitembelea awamu ya pili ya ujenzi wa barabara za mwendokasi kutoka Gerezani hadi Mbagala na kuagiza utekelezaji wake ufanyike kwa kuzingatia muda uliopangwa ili kuwaondolea adha wanayopata wakazi wa Mbagala.

## NEMC yajitosa elimu ya kulinda vyanzo vya maji

**Na Mwandishi Wetu, MAKETE**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema litashirikiana na viongozi na wananchi wa Wilaya ya Makete kulinda vyanzo vya maji kwa sababu vyanzo hivyo ni muhimu kwa taifa.

Akizungumza na wanakijiji wa Kijiji cha Kiligano, Kata ya Kitulo, Wilaya ya Makete, Mkurugenzi Mkuu wa baraza hilo, Dk Dk.Samuel Gwamaka, alisema mbali ya ukweli kwamba maji kutoka Wilaya ya Makete ni muhimu yafike Mto Rufiji, uchafuzi wa vyanzo vya maji unaweza ukasababisha madhara makubwa kwa binadamu na viumbe vya majini.

"NEMC itashirikiana kwa karibu na wadau wa mazingira na uongozi wa wilaya kutoa elimu kwa wananchi kwa wakati stahiki ili kutokomeza uharibufu wa vyanzo vya maji," alisema Dk. Gwamaka.

Alieleza kuwa vyanzo vya maji vilivyomo Wilaya ya Makete vinavyotiririsha maji Mto Ruaha ni muhimu sana kwa uzalishaji wa umeme nchini, kwani umeme utakaozalishwa Mto Rufiji utawezesha Watanzania wengi kupata umeme kwa bei rahisi.

"Serikali inatekeleza mradi wa kufua katika bwawa wa kufua umeme katika mradi wa Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115. Lakini kama hatutatunza vyanzo vya maji vya wilayani humu na kwingineko tutashindwa kufikia lengo hilo," alisema Dk. Gwamaka.

Dkt. Gwamaka ambaye alifuatana na Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Prof. Esnati Chaggu, pamoja na maofisa wengine wa NEMC, alisema wananchi waelimishwe umuhimu wa rasilimali maji katika kujiletea maendeleo na katika kuleta maendeleo ya taifa.

Mapema Prof.Chaggu aliupongeza uongozi wa Hifadhi Kitulo kwa kushirikiana kwa karibu na wananchi waishio karibu na hifadhi hiyo na kwa namna wanavyotunza hifadhi hiyo.

Prof. Chaggu amewaomba wasimamizi wa hifadhi hiyo kutumia uzoefu na maarifa yao kueneza elimu ya utunzwaji wa mazingira kwa wananchi, kwani elimu hiyo itasaidia vyanzo vya maji kutunzwa.

Atian Sanga, mkazi wa kijiji cha Ujuni kilicho karibu na Hifadhi ya Kitulo alisema wakulima wengi wa eneo hilo hawana elimu ya kutosha juu ya utunzaji wa mzingira na vyanzo vya maji na kuomba mamlaka husika zitoe elimu hiyo.

Naye Meneja Mazingira wa Wilaya ya Makete, Raphael Kalongola, alisem Wilaya ya Makete ina vyanzo 966 vinavyojulikana, lakini maji yanapotiririka kuelekea Wilaya ya Mbalali hayatumiki vizuri na matokeo yake ni kiasi kidogo cha maji kinafika Mto Ruaha.

## Wakulima 83,000 kupata mbolea bure

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA 83,000 nchini watanufaika kwa kupata mbolea bure kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mpunga na mahindi.

Uwezeshaji huo utafanywa na kampuni ya mbolea ya YARA Tanzania, ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Winston Odhiambo, amesema zaidi ya tani 12,500 za mbolea ya Yara-Mila Cereal yenye thamani ya shilingi bilioni 16.5 zitagawiwa kwa wakulima wadogo.

"Uzinduzi wa mpango hu unaojulikana kama 'Action Africa' utafanywa Alhamisi wiki hii (kesho) na Waziri wa Kilimo,Japhet Hasunga," alisema Odhiambo na kuongeza kuwa Yara

Tanzania ambayo ni kampuni tanzu ya Yara International ASA ya Norway ni mdau muhimu katika maendeleo ya sekta ya kilimo.

Odhiambo alisema chini ya mpango huo, mkulima atahitajika kujisajili kupitia namba *149*46*16# ambapo kitambulisho cha mpigakura na cha taifa kitatumika katika kukamilisha usajili sambamba na kuzawadiwa mbolea.

"Mpango huu utawasaidia wakulima wadogo wa mahindi na mpunga kuongeza uzalishaji wa mazao hayo na kuondokana na tatizo la njaa," alisema na kuwaomba wakulima kuchangamkia fursa hiyo.

## Wavuvi kukopeshwa kudhibiti uvuvi haramu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya Kilimo (TADB), Japhet Justine, amemhakikishia Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi hususani wa Bwawa la Nyumba ya Mungu ili kuondokana na uvuvi haramu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ziara alipotembelea Bwawa la Nyumba ya Mungu na kujionea shughuli zinazofanywa na wavuvi akiwa na Waziri Mpina, Justine alisema benki hiyo imedhamiria kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya uvuvi kwa kuwawezesha wavuvi zana za kisasa.

"Kumekuwa na matumizi ya zana zisizo na ubora katika shughuli za uvuvi, hali ambayo imesababisha mazalia ya samaki kupungua na kuzorotesha mapato katika sekta hiyo, TADB tutaendelea kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu wavuvi ili kuwa na uvuvi endelevu kote nchini," alisema.

Justine alisema milango ipo wazi kwa benki na taasisi za fedha kushirikiana na benki hiyo ili kupunguza changamoto zinazoikabili sekta ya uvuvi na ufugaji ambazo zimeajiri Watanzania wengi.

Waziri Mpina alipongeza hatua zinazochukuliwa na TADB na kuwataka wavuvi kutumia vyema mikopo inayotolewa na benki hiyo ili kuleta maendeleo ya kweli hapa nchini.

"Rasilimali za uvuvi zinatakiwa kulindwa na kila mwananchi, tunaipongeza TADB kwa uzalendo wao wa kuwawezesha wavuvi ili kuondokana na uvuvi wa kutumia zana hafifu ambazo zimeleta athari hasi katika sekta hii kwa kupunguza mazalia ya samaki," alisema Mpina.

# Ajali ya Coaster na basi ilivyoua wawili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATU wawili wamefariki dunia na 19 kujeruhiwa baada ya gari waliokuwa wakisafiria namba T.883 DEF aina ya Toyota Coaster kugongana na basi aina ya Yutong lenye namba T.448 DDL, mali ya kampuni ya Freys Coach.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salum Hamduni, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 8:40 mchana eneo la njia panda ya Mondi barabara kuu ya Arusha-Babati.

**Basi la Yutong lilikuwa likitokea Arusha kwenda Singida na Toyota Coaster ilikuwa ikotokea Monduli.**

Alisema basi la Yutong lilikuwa likitokea Arusha kwenda Singida na Toyota Coaster ilikuwa ikotokea Wilaya ya Monduli kwenda Arusha.

Alisema waliofariki ni mwanaume mwenye umri kati ya miaka (25 hadi 35) na mwanamke mwenye miaka kati ya (30 hadi 35), ambao majina yao hayajajulikana.

Aidha, alisema baada ya ajali hiyo majeruhi wote 19 waliokuwa kwenye gari Coaster walifikishwa Hospitali ya Jeshi ya Monduli ambapo baadaye walihamishiwa Hospitali ya Rufani ya Mount Meru.

Kamanda Hamduni alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa Coaster kushindwa kuchukua tahadhari za usalama barabarani wakati akitokea njia ndogo ya Monduli kuingia barabara kuu ya Arusha-Babati.

Alisema miili imehifadhiwa Hospitali ya Jeshi Monduli kwa uchunguzi zaidi wa daktari.



Wananchi wakiangalia gari lililomshinda dereva na kuingia kwenye mtaro katika eneo la Kawe, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Agizo Magufuli kujengwa kiwanda Rukwa latekelezwa

**Na Mbaraka Kambona**

RAIS John Magufuli alipofanya ziara mkoani Rukwa mwaka jana, moja ya maelekezo yake kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kuhakikisha kunaanzishwa kiwanda cha kuchakata samaki, ili kuwasaidia wavuvi wa maeneo hayo kupata soko la uhakika la samaki wao.

Kufuatia agizo hilo, Kampuni ya Alpha Tanganyika Flavour kupitia ushirikiano kutoka kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi imefanya uwekezaji katika sekta ya uvuvi kwa kuanzisha kiwanda cha kuchakata samaki ambacho kwa sasa kinamalizia ukarabati wake kabla ya kuanza kazi mwishoni mwa Septemba mwaka huu.

Hayo yalifahamika, baada ya Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, alipofanya ziara ya kukagua ukarabati wa kiwanda hicho kilichopo wilayani Sumbawanga, Agosti 13, 2020.

Akiwa katika kiwanda hicho, Dk. Tamatamah alisema Rais Magufuli alipofanya ziara yake mwaka jana katika mkoa huo moja ya maelekezo yake kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kuhakikisha kuwa katika mkoa huo kunaanzishwa kiwanda cha kuchakata samaki ili kuwaondolea kadhia ya masoko wanayoipata wavuvi wa maeneo hayo na mikoa ya jirani.

"Leo nimekuja na wataalamu wangu kukagua ukarabati unaoendelea katika kiwanda hiki cha Alpha, ambapo ukikamilika na kiwanda hiki kuanza kazi, kitatoa ajira zaidi ya 100 kwa wananchi na vile vile kitachangia kuongeza mapato ya serikali," alisema Dk. Tamatamah.

Dk. Tamatamah aliongeza kuwa kiwanda hicho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuchakata tani 20 za samaki ambazo bidhaa zake zitauzwa ndani ya Tanzania na vile vile katika soko la Marekani, hivyo kitasaidia nchi kupata fedha za kigeni.

Alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Alpha Tanganyika Flavour, Alpha Nondo, kwa kuamua kufanya uwekezaji huo.

Nondo aliishukuru serikali kwa ushirikiano mkubwa wanaompatia, huku akisema kiwanda hicho kitakuwa ni jibu kwa Rais Magufuli na wavuvi waliokuwa wanahangaika na soko la kupeleka samaki wao.

Naye Katibu Tawala Msaidizi, mkoani Rukwa, Ocrani Chengula, alisema kwa muda mrefu mkoa huo ulikuwa unahangaika kupata kiwanda cha kuchakata samaki ili kuwasaidia wavuvi kupata masoko ya uhakika.

# Kanyasu aelekeza chuo kupewa kitalu kuwinda

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa kitalu cha uwindaji wa kitalii kwa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka, ili kitumike kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wanaosomea masomo ya uwindaji bingwa.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizindua bodi ya magavana ya chuo hicho kilichopo Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro. Kanyasu alisema kitalu hicho kitakisaidia chuo hicho kuzalisha wataalamu wenye sifa.

Alisema kwa sasa mabingwa wa uwindaji wa kitalii wanaofanya kazi hiyo nchini ni raia wa kigeni na baadhi ya wazawa waliopo ni wazee.

**Kwa sasa mabingwa wa uwindaji wa kitalii wanaofanya kazi hiyo nchini ni raia wa kigeni na baadhi ya wazawa waliopo ni wazee.**

Alisema kitalu hicho kitachochea kupata wataalamu wa kutosha ili kukabiliana na uhaba wa wataalamu wa fani hiyo.

Aidha, Kanyasu alisema chuo hicho kitasaidia kukabiliana na wafugaji wanaoingiza vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa vile vitalu vingi bado vipo wazi, hali inayosababisha wafugaji wengi kuingiza mifugo.

Pia, alisema kitalu hicho hakitasaidia wahitimu pekee kufanya mafunzo kwa vitendo bali itasaidia wanyamapori kuwa salama kwa sababu chuo hicho kitakuwa na jukumu la kupambana na tatizo la ujangili.

Alimpongeza Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Faustine Bee, kwa kuchaguliwa kwa awamu ya pili ya kuiongoza pamoja na magavana wa bodi kwa asilimia kubwa kuteuliwa tena kuendelea kukitumikia chuo hicho.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Jaffari Kidegesho, alisema kwa sasa wanafunzi wamekosa maeneo ya kufanyia mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya uwindaji wa kitalii.

Alisema mwanzo chuo hicho kilikuwa kikiyatumia mapori ya akiba kwa ajili ya mafunzo hayo ila kwa sasa mapori hayo yamepandishwa hadhi na kuwa hifadhi za taifa, hivyo katika hifadhi hizo hakuna shughuli za kibinadamu zinazoruhusiwa kufanyika kwa mujibu wa sheria.

Prof. Kidegesho alisema kitalu hicho kitasaidia kufanya mafunzo kwa vitendo, hivyo kutasaidia kuwaandaa wahitimu wenye sifa kulingana na mahitaji ya soko

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, alikitaka chuo hicho kuboresha mtaala wa mafunzo hayo ili kuzalisha wataalamu watakaoweza kujibu changamoto za soko.

Mkuu wa Wilaya ya Kilimanjaro, Alhaji Rajabu Kundya, alisema suala la uhifadhi na utalii limekuwa na mchango mkubwa sana kwa uchumi wa Taifa hali iliyosababisha Tanzania kukua kiuchumi.




Mwasisi na Kiongozi Mkuu wa Huduma ya Tanzania Itubu, Dk. Kennedy Mwasumbi (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu kongamano la uamsho la kuombea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu. Kulia mratibu wa kongamano hilo, Askofu Alfred Juma na Askofu wa Huduma ya Urejesho wa Pentekoste, William Mtenga. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Naibu Mufti ataka amani idumishwe

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

NAIBU Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Mahmoud Mussa Wadi, amewataka vijana kisiwani Pemba kusimamia na kudumisha amani iliyopo nchini hasa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Akizungumza na vijana hao kwenye kongamano la amani na utulivu kwa vijana, lililofanyika Uwanja wa Michezo Gombani Chakechake, Wadi alisema, historia ya amani ilianza tangu mwanzo wa dunia hivyo ni vyema kuiendeleza.

Alisema kipindi cha uchaguzi ni kigumu sana, hivyo ipo haja kwa vijana kuiendeleza amani iliyopo na kuisimamia kwani bila kuwapo amani hakuna furaha wala maendeleo, badala yake ni kuharibu maendeleo yalishapatikana kwa muda mrefu, huku kuendeleza upya ni vigumu.

Alieleza kuwa, vijana ni watu muhimu katika kusimamia na kuimarisha amani na ndio maana wakaanza kuwaelimisha wao, kwani yanayosemwa katika jamii huamsha hisia za watu.

## Wapewa siri kuepuka gharama za matibabu

**Na Beatrice Shayo**

MFUKO wa Taifa ya Bima ya Afya (NHIF), umewashauri wananchi kuacha tabia ya kusubiri kuugua na kuona gharama za matibabu zimekuwa kubwa ndipo wanakwenda kukata bima ya afya.

Ushauri huo ulitolewa na Meneja Uhusiano wa NHIF, Anjela Mziray, wakati wa mkutano mkuu na uchaguzi wa viongozi wa klabu ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam (DCPC) mwishoni mwa wiki.

Alisema ni muhimu kwa wananchi kutambua dhana ya bima ya afya badala ya kusubiria wanapoumwa na kuona gharama za matibabu zimekuwa kubwa na kuanza kutafuta bima ya afya.

Mziray alisema wamejiwekea utaratibu wa kuwa bila kufanya hivyo, mfuko utakufa kwa sababu atakuja mgonjwa wa saratani anatakiwa kuanza matibabu ndipo anakata bima ya kifurushi hata akikata ya Sh. 1,000,000 akiitumia kwa miezi miwili bado haitoshi.

# Kigamboni yabanwa nyumba za watumishi

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Joseph Nyamhanga, ametoa siku 90 kwa Manispaa ya Kigamboni kukamilisha ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi wa wilaya hiyo.

Nyamhanga alitoa agizo hilo, juzi jijini Dar wes Salaam, alipotembelea mradi huo wa ujenzi wa nyumba za watumishi 25 kati ya hizo, moja inajengwa na halmashauri na kusema kuwa lengo ni kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Akiwa katika ziara yake ya kutembelea miradi mbalimbali ya kimkakati iliyopo jijini Dar es Salaam, ukiwamo wa Kigamboni, alisema hakuna sababu ya mradi huo kucheleweshwa kwa kuwa tayari serikali ilishatoa fedha ili kukamilisha.

Alisema ujenzi wa nyumba hizo 24 ulitokana na agizo alilolitoa Rais John Magufuli, Februari 11 mwaka huu, wakati akizindua jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa wilaya hiyo na kuagiza ujenzi wa nyumba hizo ukamilike haraka ili kuwaondolea usumbufu wafanyakazi na wananchi wilaya hiyo.

"Mimi najitolea kuwa meneja wa mradi huu ili nihakikishe kuwa ujenzi unamalizika mapema, nataka ukamilike ndani ya muda uliopangwa ili wafanyakazi wenu wahamie hapa haraka iwezekanavyo," alisema Nyamhanga.

Alisema ni lazima suala hilo litekelezwe kama ilivyopangwa na kwamba ikifika Novemba mwaka huu wafanyakazi hao ambao kwa sasa baadhi yao wanaishi katika nyumba za Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na wengine nje ya manispaa hiyo wahamie katika nyumba hizo.

Akitoa taarifa za mradi huo unaogharimu serikali Sh. bilioni 2, Mkurugenzi wa Manispaa hiyo ya Kigamboni, Erasto Kiwale, alisema maandalizi ya ujenzi huo yamekamilika ikiwa ni pamoja na kumpata mkandarasi atakayejenga nyumba hizo.

Alisema awali ilipangwa kujenga nyumba 20, lakini kutokana na mchanganuo walioufanya waliona fedha hizo zinatosha kujenga nyumba 24 ambazo wanaamini kukamilika kwake kutatoa changamoto ya makazi inayowakabili watumishi wake.

"Wizara imeanza kuleta fedha za utekelezaji kwa awamu, awamu ya kwanza zimeshaletwa Sh. bilioni 1.499 na matarajio yetu ujenzi huu utachukua muda wa siku 90 kuanzia sasa na hivyo kutoa fursa ya watumishi kuhamia eneo hili," alisema Kiwale.

## Ukinzani kikatiba unavyokwamisha wagombea huru, mikataba Afrika

Ukurasa 12





Ukurasa 13

## Ndivyo NEC 'ilivyojinasibu' kufanikisha uchaguzi 2020

**siasa**

JUMATANO JAGOSTI 19, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Kampeni za uchaguzi chachu ya kudumisha amani na utulivu



viongozi na wafuasi wa CCM wakiwa katika moja ya mikutano ya kampeni. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Dk. Enock Mlyuka**

KIPENGA cha uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani pamoja na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kimepulizwa na sasa ni mchakato wa vyama kupata wagombea kabla ya kupitishwa na vyombo vilivyopewa dhamana ya kusimamia kazi hiyo.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na ile ya Zanzibar (ZEC) ndizo zilizopewa dhamana ya kusimamia mchakato mzima wa uchaguzi na kuhakikisha unakuwa huru na wa haki. NEC inasimamia uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani wakati ZEC mamlaka yake ni kwa uchaguzi wa Raia wa Zanzibar na Wawakilishi.

Hivi sasa vyama vyote viko katika hatua ya kuteua wanachama watakaopeperusha bendera kwenye uchaguzi huo ambao Watanzania, wale waliojiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura, watatumia haki yao ya kidemokrasia kuchagua watu wanaoona wanafaa katika nafasi zinazowaniwa ifikapo Oktoba 28, mwaka huu.

Katika kuelekea tarehe hiyo mahusus, Watanzania wanapaswa kufahamu kuwa tendo hili kubwa na la kihistoria katika nchi. Kila mwananchi, kwa imani yake, anao wajibu wa kumwomba Mungu kwa bidii ili nchi iendelee kuwa kisiwa cha amani na utulivu.

> Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na ile ya Zanzibar (ZEC) ndizo zilizopewa dhamana ya kusimamia mchakato mzima...

Tanzania imekuwa ikitajwa kuwa nchi ya kwanza kwa utulivu na amani katika ukanda wa Afrika Mashariki na pia ni moja ya nchi chache za mfano katika nchi zilizo kusini mwa jangwa la sahara.

Sifa hii njema inapaswa kutunzwa na kulindwa na wananchi wote pasipo kujali tofauti za kiitikadi. Nchi hii ni ya Watanzania wote na si mali ya chama au kikundi fulani cha watu. Kama yapo mazuri au mabaya, ni ya Watanzania wote, hivyo Tanzania ikiwa salama, Watanzania wote watakuwa salama na maendeleo yatakuwapo.

Katika kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu, jambo la msingi la kujifunza ni kutoka kwa nchi nyingine nje na ndani ya Bara la Afrika, ambazo amani na utulivu vilipoondoshwa, vita na mauaji vilitokea na kuangamiza nchi na ustawi wake.

Baadhi ya nchi zimegeuka kuwa magofu kwa sababu ya vita vya wenyewe kwa wenyewe visivyokoma. Wanapoendelea na migogoro, mataifa mengine ya nje ya Afrika hutumia mwanya huo kupora mali za nchi husika na wananchi kuishi maisha duni.

Kumwaga damu za watu wasio na hatia ni laana kwa nchi. Mungu huchukizwa sana na hali kama hiyo na kwa kweli hawezi kunyamaza wakati wote. Kuna wakati Mungu hulazimika kuiadhibu nchi na watu wake kwa sababu ya uharibifu wa uumbaji wake na kupuuzwa kwa utaratibu mzuri wa kuishi aliouweka duniani.

Kwa mantiki hiyo, amani na utulivu ambavyo Watanzania wanavifurahia sasa, hawana budi kufahamu kuwa vimejengwa kwa miaka mingi. Siku zote kujenga ni kazi lakini kubomoa ni rahisi. Pia gharama ya kurejesha utulivu na amani vilivyopotea ni kazi kubwa.

**INAENDELEA UK.12**

# Ukinzani kikatiba unavyokwamisha wagombea huru, mikataba Afrika



Wakili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Beatrice Mpangala, akizungumza na wadau wakati wa mkutano wa tafakuri ya uchaguzi mkuu wa 2020. **PICHA: MWANDISHI WETU.**

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI imebakia miezi miwili kufikia kilele cha uchaguzi mkuu wa 2020, wapo wagombea ubunge na urais ambao walitamani kuingia kwenye kinyang'anyiro lakini wanakwamishwa na vyama vyao, kwa maelezo kuwa hawakubaliki au wakae pembeni kupisha wengine.

Wasingekwama kama taifa lingekuwa na kipengele kinachoruhusu wagombea huru au binafsi, hatua ambayo ingewawezesha wasio na vyama kuingia ulingoni bila kikwazo.

Kigingi ni katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 ambayo ibara ya 39(1)c inapigilia msumari kuwa mgombea yeyote wa ubunge au urais ni lazima awe amependekezwa na chama cha siasa, hivyo, hakuna kugombea nje ya utaratibu huo.

Kadhalika sheria ya uchaguzi mkuu ya mwaka 2010 inasisitiza kuwa lazima wagombea wawe ni madiwani, wabunge au rais watokane na vyama vya siasa vilivyosajiliwa na kutambuliwa kisheria.

Hivyo bila katiba kuipitia tena katiba raia hawawezi kujitosa kwenye uchaguzi kama wagombea huru au binafsi wa ubunge, udiwani au urais.

Pamoja na hilo ibara ya 41 (7) na 42 ya katiba ya Tanzania inaeleza kuwa baada ya matokea ya rais yaliyotokana na uchaguzi mkuu kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, hayawezi kuhojiwa mahakamani.

Vifungu hivyo vya kukataza mgombea huru na kupinga matokeo ya urais mahamakani vimekuwa na athari si kwa wagombea wa nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi mkuu au kupinga matokeo ya urais kama hawajaridhika bali pia vinaikwamisha Tanzania kusaini mikataba ya Umoja wa Afrika (AU), kwa vile inaonekana kuwa vinakinzana na katiba ya nchi.

Hayo ni miongoni mwa mambo yanayojadiliwa katika mkutano na wanahabari wa kutafakari uchaguzi mkuu wa 2020, unaoandaliwa na asasi ya vijana ya Tanzania Youth Vision Association (TYVA).

Mkutano huo wa tafakari unawashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB)), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ActionAid na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Wakili wa Serikali Beatrice Mpangala, anazungumzia suala la vipengele hivyo vinavyokataza wagombea huru na kile cha kuzuia kupinga matokea mahakamani pamoja na taathira zake kwa mikataba ya AU akisema ndivyo

> Aidha, imeishauri serikali kuhusu usafi magerezani Bara na Visiwani kwenye vyuo vya mafunzo na kushauri kuondolewa utaratibu wa wafungwa na mahabusi kutumia ndoo kujisaidia badala yake wajengewe vyoo na yote yametekelezwa. Anasema wakati wa uchaguzi inashauri mambo mengi na hata kutoa elimu ya umuhimu wa demokrasia na uchaguzi kwa wananchi.

sababu kubwa, inayozuia Tanzania isisaini wala kuridhia mkataba wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora (ACDEG).

Anaeleza kuwa serikali inachelea kuusaini na kuuridhia kwa vile unapingana na katiba yake kwenye vipengele hivyo.

Mpangala, anakumbusha kuwa kusaini mkataba huo kunamaanisha Tanzania itaruhusu kuwa na wagombea huru na pia kwa wasioridhika na matokeo ya urais baada ya uchaguzi mkuu kutangazwa na NEC kumpinga rais mshindi mahakamani.

Anakumbusha kuwa kusaini na kuridhia ACDEG kutakuwa ni kukinzana na vipengele 41 and 42 vya katiba kwa hiyo mijadala na mapendekezo zaidi kwa serikali yanahitajika ili kupata namna bora ya kuishauri kuuridhia mkataba huo unaolenga kudumisha demokrasia Afrika, utawala bora na uchaguzi huru na haki pamoja na kuheshimu haki za watu na za binadamu.

Suala la katiba kukataza matokeo ya urais kupingwa mahakamani lilifikishwa katika Mahakama ya Haki za Binadamu na za Watu ya Afrika mjini Arusha na wakili Jebra Kambole, akitaka kipengele hicho kifutwe.

Mahakama hiyo ilihukumu kwa kuitaka Tanzania kurekebisha baadhi ya vipengele vya katiba vinavyozuia matokeo ya urais kupingwa mahakamani. Hukumu hiyo ilimaanisha kiondolewe na kuruhusu mashtaka kufunguliwa dhidi ya matokeo ya urais.

Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika iliielezea katiba kuwa inakiuka Ibara ya 2 na ya 7 (1) cha mahakama hiyo kinaeleza kuwa endapo mtu hataridhika na matokeo ya urais, ana haki ya kukata rufani kwa kufikisha kesi mahakamani kupinga matokeo husika.

Hata hivyo, Mpangala anakumbusha kuwa Tanzania imejiondoa na si mwanachama wa Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu ya Afrika, hatua inayokwamisha utekelezaji wa uamuzi ya mahakama hiyo.

Aidha, anaeleza kuwa hakuna jambo baya kwenye mkataba wa ACDEG na kwamba Tanzania inaweza kuusaini na kuuridhia kwa masharti kuwa haikubaliani na vipengele vyote kwa kuainisha vile ambavyo haivikubali kwa kuwa vinakinzana na katiba ya jamhuri.

Kwa mujibu wa taarifa za mtandao wa Idara ya Siasa ya AU , hadi Juni, 2019 kati ya mataifa 55 wanachama wa AU nchi tano ambazo ni Tanzania, Misri, Eritrea, Morocco na Libya zilikuwa hazijasaini wala kuridhia mkataba wa ACDEG.

Aidha, wanachama 46 wa AU wameusaini mkataba, wakati 34 wameusaini na kuuridhia kwa mujibu wa taarifa za hadi Juni mwaka jana.

**KUTEKELEZA ACDEG**

Licha ya kutosaini wala kuridhia ACDEG, Tanzania imekuwa mstari wa mbele kusimamia demokrasia, uchaguzi huru na utawala bora na kuheshimu haki za binadamu, washiriki wa mkutano huo wanaambiwa.

Mtafiti Mkuu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Fransisco anasema mojawapo ya majukumu yanayotajwa na Umoja wa Afrika ni kuheshimu haki za watu na za binadamu na utawala bora na hilo Tanzania inalizingatia.

Anasema kwa mfano THBUB inatembelea magereza na kushauri mambo mbalimbali na mojawapo ni kuitaka serikali kubadilisha sare za wafungwa badala ya kuvaa kaptula wavae suruali.

Aidha, imeishauri serikali kuhusu usafi magerezani Bara na Visiwani kwenye vyuo vya mafunzo na kushauri kuondolewa utaratibu wa wafungwa na mahabusi kutumia ndoo kujisaidia badala yake wajengewe vyoo na yote yametekelezwa. Anasema wakati wa uchaguzi inashauri mambo mengi na hata kutoa elimu ya umuhimu wa demokrasia na uchaguzi kwa wananchi.

Kwa upande wa TAKUKURU, Matai Kilumbi, anasema Afrika inasisitiza vita dhidi ya rushwa na matumizi bora na endelevu ya mali za umma na rasilimali za nchi yote haya yanazingatiwa na wakati huu wa uchaguzi taasisi iko mstari wa mbele kusimamia haki na usawa wakati wa kampeni kwa kuzuia na kudhibiti ushawishi, utoaji na upokeaji wa rushwa.

Aidha, anazungumzia suala la kupiga vita rushwa kwani inakwamisha demokrasia na uchaguzi huru akisema kuwa TAKUKURU inafuatilia, kudhibiti na kuzuia ushawishi, utoaji na upokeaji hongo wakati wa uchaguzi.

Kilumbi anasema haiwezekani kiongozi bora akatokana na kutoa rushwa hivyo wanahamasisha wananchi kuwaripoti wanaowashawishi kuwachagua kwa kupewa fedha.

# Ndivyo NEC 'ilivyojinasibu' kufanikisha uchaguzi 2020



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufaa, Semistocles Kaijage.

**Sabato Kasika**

IKIWA imebakia takribani miezi miwili Watanzania wawachague viongozi wao kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Jumatano Oktoba 28, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeainisha mambo kadhaa muhimu yatakayofanikisha jukumu hilo ikiwa ni pamoja na kudumisha amani.

Aidha, imetoa ahadi na kuwahakikishia wananchi kuwa itasimamia uchaguzi kwa kuzingatia katiba, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazosimamia uendeshaji wa uchaguzi.

Lengo la kufanya hivyo likiwa ni kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru, wa wazi, wa haki na wa kuaminika, hivyo itaweka mazingira sawa ya ushindani kwa wagombea na vyama vyote vya siasa vitakavyoshiriki. Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, ndiye aliyesema hayo katika mkutano wake na viongozi wa dini uliofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita.

"Ahadi ya tume kwenu ni kwamba itasimamia uchaguzi kwa kuzingatia katiba, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazosimamia uendeshaji wa uchaguzi, lengo likiwa ni unakuwa huru, wa wazi, wa haki na wa kuaminika.

Pia tume inawaomba mhubiri amani na pia kuwahimiza viongozi wa vyama vya siasa kuheshimu, kutii, kuzingatia sheria za nchi, na kanuni za tume, ili uchaguzi uwe wa utulivu na amani," anasema Jaji Kaijage.

Kutokana hilo, anawaomba viongozi wa dini kuhimiza kampeni zitakazoanza rasmi Agosti 26 mwaka huu, ziwe za kistaarabu ambazo zitaepusha vitendo vya uvunjifu wa amani ya nchi.

"Nitumie nafasi hii kuwaomba muendelee kuhubiri amani, hasa wakati wa kipindi cha kampeni, msichoke kuwasisitiza wagombea, wadau na wananchi kwa ujumla kuheshimu, kutii na kuzingatia katiba ya nchi," anasema.

**UZOEFU WA NEC**

Jaji Kaijage kipindi cha kampeni kinakuwa na joto kali la kisiasa linalotokana na baadhi ya watu kukosa uvumilivu wa kisiasa, hali ambayo inaweza kuhatarisha amani na utulivu wa nchi.

> Ninapenda kutoa rai kwenye kuhimiza waumini wenu na kuwasihi kufanya kampeni kistaarabu na hivyo kuepuka kufanya vitendo vitakavyosababisha uvunjifu wa amani na utulivu wa nchi yetu," anasema.

"Ninapenda kutoa rai kwenye kuhimiza waumini wenu na kuwasihi kufanya kampeni kistaarabu na hivyo kuepuka kufanya vitendo vitakavyosababisha uvunjifu wa amani na utulivu wa nchi yetu," anasema.

Mbali na hilo, anawaomba viongozi wa dini kuliombea taifa katika kipindi hiki muhimu, ili amani na uvumilivu vitawale, na kwamba tume hiyo ina matumaini makubwa ya kufanikisha uchaguzi huo.

Anasema, matumaini hayo yanategemea ushiriki wa viongozi hao katika hatua zote zilizosalia hadi kufikia Oktoba 28 ambayo itakuwa ni siku ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani.

"Ahadi ya tume kwenu ni kwamba itasimamia uchaguzi kwa kuzingatia katiba, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazosimamia uendeshaji wa uchaguzi, lengo likiwa ni unakuwa huru, wa wazi, wa haki na wa kuaminika, " anasema.

Jaji huyo anasema utaaminika, kwa vile tume itaweka mazingira sawa ya ushindani kwa wagombea na vyama vyote vya siasa vitakavyoshiriki.

**VYAMA VISHIRIKI**

Kwa mujibu wa tume hiyo, hadi kufikia Agosti 11, mwaka huu, ilikuwa imeshatoa fomu za kuomba uteuzi wa kuwania urais kwa wagombea kutoka vyama 16 vya siasa, kati ya 19 vyenye usajili wa kudumu.

Mkurugenzi wa tume hiyo, Dk. Wilson Mahera, anavitaja vyama hivyo kuwa ni AAFP, ACT-Wazalendo, Ada Tadea, ADC, CCM, CCK, Chadema, Chaumma, CUF, DP, Chama cha Demokrasia Makini, NRA, NCCR- Mageuzi, SAU, UMD na UPDP.

Aidha, anahimiza umuhimu wa maslahi ya taifa kwanza, na ushabiki wa vyama vya siasa baadaye, hivyo wagombea hawapaswi kutumia lugha ya matusi, vitisho na kejeli, kwa kuwa vinachochea fujo.

"Vitendo hivyo vinasababisha uvunjifu wa amani, hivyo maslahi ya taifa yawe ya kwanza na ushabiki wa vyama baadaye, na tuendelee kuombea amani na utulivu wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi," anasema Dk. Mahera.

WOSIA VIONGOZI WA DINI

Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Alhad Mussa Salum anasema, viongozi wa dini wana nafasi kubwa katika kuimarisha amani kwa kuwa wananchi ni waumini wao, kwenye misikiti na makanisani.

"Yaliyozungumzwa na mwenyekiti wa tume, tunapaswa kuyachukua na kuwaeleza waumini kuhusu namna bora ya kushiriki katika uchaguzi mkuu kwa kufuata nidhamu na taratibu," Sheikh huyo.

Kwa upande wake Mchungaji wa Kanisa la Movanian, Jimbo la Mashariki Neema Kashiririka, anasema ni vyema viongozi wa dini kuwaeleza waumini umuhimu wa amani.

Amani na utulivu vinapokuwapo watachagua kiongozi mzuri, hivyo ni wajibu wetu viongozi wa madhehebu ya dini kuhimiza umuhimu wa amani na utulivu kwa manufaa ya taifa letu," anasema Kashiririka.

**KUCHAFUANA KISIASA**

Imekuwa ni kawaida kila unapofanyika uchaguzi, baadhi ya wanasiasa kufanya siasa za majitaka kwa 'kushambulia' wenzao kwa maneno makali na hata kuwasingizia mambo ambayo hayafai.


Hivyo, nchi inapoelekea katika uchaguzi mkuu, wanasiasa waweke kando siasa za aina hiyo, ambazo huitwa siasa za majitaka, kwa kuwa zinachagiza mipasuko na mivutano isiyo na tija kwa taifa.

Wanasiasa kutumia muda mwingi kunadi sera na ilani za vyama vyao katika kampeni ni njia nzuri ya kufikia kile Nec inachokitaka ili kufanikisha uchaguzi huo, si kuanzisha malumbano bila kujenga hoja za kushawishi wapigakura.

Hivyo, kila mwanasiasa ana nafasi ya kushiriki katika uchaguzi bila kuchafua hadhi na heshima ya wenzake na ya kitaifa

# KOFI ANNAN

## ■Mwafrika namba 1 kuongoza UN
## ■Anang'ara kusaka amani duniani
## ■18.8.2018 aliaga dunia




Koffi Anna akiongoza mikutano ya UN enzi za uongozi wake. PICHA: MTANDAO.

**Na Mwandishi Wetu**

KOFI ANNAN ndiye Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuanzia mwaka 1996 - 2006. Katibu Annan na Umoja wa Mataifa kwa pamoja walipata Tuzo ya Amani ya Nobeli mwaka 2001.

Jana Agosti 18 ni siku aliyofariki kiongozi huyo, anayekumbukwa na mataifa mengi kwa kuhangaikia amani na maridhiano duniani. Ndiye aliyekuwa mwanzilishi na mwenyekiti wa Kofi Annan Foundation na pia Mwenyekiti wa Elders, Shirika la Kimataifa lililoanzishwa na Rais wa Kwanza mweuzi wa Afrika Nelson Mandela.

Annan aliyefariki Agosti 18, 2018 akiwa na miaka 80, alizaliwa Aprili 1938 nchini Ghana na kuaga dunia Agosti 18, 2018 akiwa jijini Bern Uswisi. Alipoondoka UN mwaka 2006 alimwachia kijiti cha uongozi wa Umoja wa Mataifa Ban Kimoon, ambaye naye amemkabidhi Antonio Guterres.

Annan alikuwa ni Mwafrika wa kwanza kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, akihudumu mihula miwili kuanzia mwaka 1997 hadi 2006. Baadaye akaendelea kulitumikia shirika hilo kama mjumbe maalum wa Umoja wa Mataifa nchini Siria na kufanikisha kupatikana kwa suluhisho la amani la mzozo wa nchi hiyo.

MAMBO MAKUU

Kiongozi huyo aliyezaliwa mwaka 1938 huko Kumasi ambao sasa ni mji wa pili kwa ukubwa nchini Ghana, alikuwa ni pacha akizaliwa na dada yake aitwaye Efua aliyeaga dunia 1991. Mwaka 1962 alianza kufanya kazi UN huko Geneva, Uswis na kuendelea na utumishi hadi mwaka 1993 alipochaguliwa kuwa Mkuu wa Oparesheni za Kulinda Amani.

Kuanzia mwaka 1997 aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa saba wa UN na akaweka alama zisizofutika kwa kuwa kiongozi mashuhuri kwenye harakati za amani. Alikuwa mmoja wa washindi wa Tuzo la Amani ya Nobel mwaka 2001. Baada ya miaka 10 ya kazi mwaka 2006 aliondoka kwenye uongozi mkuu wa UN.

**ALIYOYAHAMASISHA**

Wakati wa kumbukumbu ya kifo chake, iliyofanyika mwaka jana , Katibu Mku wa UN Antonio Guterres, anasema Annan alisihi kila mtu asiwe mtazamaji katika maisha na kuongeza "alitutaka sote tuchukue hatua dhidi ya upendeleo, ukatili na umwagaji damu." Anamuelezea kuwa ni kiongozi aliyeutetea ushirikiano wa kimataifa kwa nguvu zote, alikuwa muumini wa UN na mfumo wa kimataifa unaofuatao kanuni.

"Na lazima niseme, kifo chake kinauma sana kwa sababu hivi sasa tunahitaji zaidi kuliko wakati wowote imani hiyo." Anasema Guterres.

Mrithi wa Annan Ban Ki-moon ambaye alipokea kijiti cha kuongoza UN mwaka 2006 anasema: "Nina uhakika kadri miaka inavyokwenda, historia itaonyesha kuwa Kofi Annan alikuwa kiongozi wa kipekee. Hakuwa na majivuno lakini alizungumza na kusikilizwa. Alikuwa kiongozi aliyeshika mambo ya zamani lakini alikuwa na dira thabiti ya kuziangazia siku zijazo."

Aliendelea kummwagia sifa akisema kuwa ni kiongozi ambaye ameacha dunia ikiomboleza kifo chake lakini pia ameipatia mchango wa kipekee ambao utakuwapo daima na utaendelea kuhamasisha, amani, haki , maridhiano na upendo.

**MALENGO YA MILENIA**

Wakati wa uongozi wa Annan kama Katibu Mkuu wa UN viongozi wa dunia walipitisha malengo ya milenia yaliyofikia ukomo mwaka 2015 na alishinda Tuzo ya Amani ya Nobel.

Katibu Mkuu huyo aliongoza na kupeleka mbele haki za binadamu na ulinzi wa amani duniani kote kwa kusisitiza kuwepo, ofisi thabiti ya maadili na kutokuvumilia kabisa ukatili wa kingono dhidi ya wanawake na watoto na kuhamasisha maendeleo endelevu.

Malengo ya Maendeleo ya Millenia yalipaswa kufikiwa mwaka 2015, yakiwa ni jukumu la Umoja wa Mataifa lililokubaliwa na wanachama kupunguza nusu ya umasikini duniani, kutoa elimu ya msingi kwa watoto wote na kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake.

**SULUHU KENYA**

Baada ya uchaguzi Mkuu wa Kenya, zilizuka vurumai za kisiasa na kiongozi huyu wa UN alitoa mchango mkubwa kuleta mapatano nchini Kenya baada ya ghasia zilizofuatia uchaguzi mkuu wa mwaka 2007.

Aliunda Tume ya Usuluhishi na kuwashirikisha viongozi kadhaa wa Afrika akiwamo hayati Rais wa Awamu ya Tatu , Benjamin Mkapa pamoja na Mstaafu Jakaya Kikwete.

Afrika Mashariki inamkumbuka kwa juhudi na kuingilia kati uhasama nchini Kenya ili kuisaidia nchi hiyo isitumbukie kwenye ghasia zilizokuwa zinatokana na matokeo yasiyokubalika ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007.

**KULINDA AMANI CONGO**

Annan anakumbukwa kwa kusaidia bila kuchoka upatikanaji wa amani ya Congo DRC.

Ulinzi wa amani ya Congo ulifuatia kusainiwa kwa mkataba wa kuacha mapigano uliofanyika Lusaka Zambia Julai 1999 ukihusisha mataifa ya Congo, Angola, Namibia, Rwanda, Uganda na Zimbabwe na kuanzia hapo Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa likaunda kikosi cha ulinzi wa amani nchini Congo maarufu kama vikosi vya kulinda amani vya Umoja wa Mataifa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (MONUSCO) ambavyo hata sasa vinaendelea na ulinzi wa amani katika eneo hilo.

***MITANDAO***

# Kampeni za uchaguzi chachu ya kudumisha amani na utulivu

**INATOKA UK.11**

Bila amani na utulivu, hakuna uhuru wa kuabudu na kufanya shughuli za kijamii na za kiuchumi katika nchi kwani migogoro na ghasia ni vikwazo vikubwa vya maendeleo. Hivyo, utulivu na amani ni muhimu katika kuwezesha maendeleo endelevu.

Kwa msingi huo, amani na utulivu katika nchi lazima vilindwe. Kila Mtanzania ni nafsi yenye haki na wajibu, hivyo suala la ulinzi na usalama wa nchi ni haki na wajibu wa kila Mtanzania na si kazi ya vyombo vya ulinzi na usalama pekee.

**KAMPENI ZIMEWADIA**

Wakati mchakato wa kupatikana wagombea watakaothibitishwa na NEC na ZEC ukikaribia, vyama vitakavyoshiriki uchaguzi huo vimeanza kutoa ratiba zao za uzinduzi wa kampeni. Hicho ni kipindi cha kila chama kunadi sera zake juu ya nini kitafanya iwapo kitapata ridhaa ya kuchaguliwa kushika dola.

Kipindi cha kampeni kikitumika vizuri, kinaweza kuijenga nchi. Lakini wakati huu ukitumika vibaya unaweza kuibomoa nchi. Kuna umuhimu mkubwa kwa wagombea wanaposimama majukwaani kujinadi, wachague maneno ya kusema kwa wananchi, huku wakitambua kuwa wanazungumza na watu wenye ufahamu.

Kutokana na ukweli huo, wagombea wanapaswa kujifunza kuzuia ndimi zao ili wasinene mabaya, uzushi na hila, mambo ambayo wananchi hawayahitaji.

Wagombea wachague maneno ya kusema kwani changamoto nyingi ambazo watu wanapitia leo ni matokeo ya maneno ambayo wamekuwa wakiyanena bila kujua athari zake kwenye maisha yao binafsi na maisha ya wengine.

Kutokana na ukweli huo, wako wanasiasa ambao hawajui athari za kutumia vinywa vyao vibaya, hivyo ni muhimu watu wakafahamu umuhimu wa kuchagua maneno ya kuzungumza kwa mustakabali wa taifa. Katika kuendesha kampeni, ni muhimu vyama vyote vya siasa vizingatie sheria za nchi , kanuni na taratibu za uchaguzi zilizotolewa na NEC na ZEC.

Wananchi wanatarajia kuwa wagombea wote watatumia vyema kipindi cha kampeni kunadi sera na ilani za vyama vyao na kwamba watazungumza masuala na si watu. Kila mgombea anatazamiwa kufanya kampeni za kistaarabu tena zenye kudhihirisha ukomavu na kujitambua.

Kwa upande wao, wananchi wana shauku ya kusikia wagombea wataifanyia nini Tanzania wakichaguliwa kuwa viongozi. Ni tumaini la Watanzania kuwa wagombea watashindana kwa hoja na si matusi na mipasho.

Wagombea wafahamu kwamba wanazungumza na wananchi wenye mwamko wa kisiasa na maendeleo, hivyo wananchi wanachotamani ni maendeleo na maisha bora. Kwa hiyo wagombea wenye ufahamu kuhusu mahitaji halisi ya wananchi na taifa, kwa vyovyote vile kampeni zao zitajikita katika kueleza sera na ilani za vyama vyao na si maneno ya uchochezi yenye kuhatarisha usalama, amani na utulivu katika jamii.

**KAULI ZA WAGOMBEA**

Mgombea anao wajibu wa kuthibitisha mbele ya wananchi kwa kauli na matendo yake kuwa anafaa kuchaguliwa kuwa kiongozi. Masuala yoyote atakayozungumza mbele ya wananchi, wakimwangalia usoni, waone uhalisia na kumaanisha kwake.

Ilani za vyama ziwe ni dira zitakazoongoza fikra na hoja za kila tendo wakati wote wa kampeni. Katika kipindi cha kampeni, wagombea hawatarajiwi kutanguliza utashi binafsi bali utashi wa vyama vyao na wananchi. Pia kampeni zihifadhi heshima za watu wengine.

Kwa mantiki hiyo, kila mgombea ana nafasi Mungu amtawale katika kampeni ili kusababisha amani na utulivu katika nchi kwani baada ya uchaguzi maisha yataendelea. Pia wafahamu kwamba wanadamu wa sasa watapita lakini mama Tanzania ataendelea kuwapo. Itampendeza Mungu na wanadamu kwamba wakiondoka duniani, wakumbukwe kwa kuacha alama ya amani na utulivu katika jamii wanazoishi.

Tanzania ni nchi ya watu wastaarabu na waungwana, hivyo, wagombea waepuke siasa za chuki na visasi. Pia waepuke kunena na kueneza uongo dhidi ya wagombea wa vyama vingine. Sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi zinapaswa kuzingatiwa na kulindwa.

Kila mgombea atambue kuwa yeye ni mwanadamu na si malaika, hivyo asitegemee ukamilifu kwa kila jambo. Kwa hiyo, wagombea wanapozungumza, wasizungumze kana kwamba wao ni wanadamu wasioweza kukosea. Jambo la msingi ni kuthaminiana, kusaidiana na kuheshimiana.

Wagombea wasimame majukwaani kwa amani, wazungumze kwa amani na kujenga jamii ya amani katika kila siku ya kampeni zao. Mwandishi wa vitabu, Robert Rabbin aliandika kwamba: "Ingawa kuna jeshi kubwa la wale wanaopendelea vurugu, lazima tuunde jeshi kubwa zaidi la watu wanaochagua amani."

Kwa kauli ya mwandishi huyo, Watanzania wanapaswa kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano. Viongozi wa dini na waumini wote, waendelee kuombea kwa mzigo nchi na uchaguzi mkuu.

Vitendo vyenye dalili ya kuondosha amani na utulivu nchini vinahitaji kukemewa kwa nguvu zote kwani watu wachache wenye nia ovu wasipodhibitiwa, wanaweza kusababisha maafa kwa taifa zima.

***• DK. Mlyuka ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na ni mwanataaluma, mtafiti na mshauri. Anapatikana kwa namba 0744 000066.***



# DC akemea uuzaji holela wa ardhi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Josephat Maganga, amewataka wananchi kutouza ardhi kiholela ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

Maganga alitoa agizo hilo jana alipozungumza na wananchi wa Kata ya Mtumba jijini hapa katika ziara yake ya kujitambulisha, kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Alisema ardhi ni kitu cha thamani na unapofanyika uamuzi wa kuiuza, wahakikishe unakuwa sahihi.

Aliwaagiza wenyeviti wa mitaa na watendaji kuwa makini na uuzaji ardhi.

"Hata kama mwananchi wa kawaida anataka kuuza eneo lake, sheria zinaturuhusu kuhoji, kwa sababu anaweza akauza ardhi hapa, mkashtukia anakuja mtu anatengeneza mambo ya baruti hapa, ukimuuliza anasema anapasua miamba hapa halafu anasababisha matatizo," alionya.

Aliwataka watendaji na wananchi kuhakikisha kabla ya kufanya uamuzi wa kuuza ardhi, washirikishe Halmashauri ya Jiji ili itoe msaada wa kisheria.

Katika hatua nyingine, Maganga ameipongeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kutenga Sh. milioni 210 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi waliotwaliwa maeneo yao.

"Ninafurahi kuona hawa wananchi 34 wanapata fidia hii na Halmashauri ya Jiji la Dodoma ninaipongeza kwa kutenga fedha hizo ambazo nimetaarifiwa zitalipwa mwezi huu," alisema.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, akijibu swali la mwananchi wa Kata ya Mtumba, Jackson Seganje, aliyetaka kujua malipo ya fidia kwa wananchi hao 34 wa eneo la Mtumba, alisema malipo hayo yatalipwa mwisho wa mwezi huu.

Mafuru ambaye ni Mkuu wa Idara ya Mipango Miji, alikiri wananchi 34 ambao maeneo yao yalitwaliwa hawakuwapo wakati wa uthamini.

"Eneo ambalo tulitwaa, tulirudia mara nne zoezi la uthamini, lakini bahati mbaya wachache wasiwapo wakati wa utekelezaji zoezi hilo, kuna kitu kinaitwa 'supplementary valuation', tutawafanyia kitabu cha pili ili wa kwanza wanalipwa kwanza na wale wengine wanalipwa baadaye," alisema.

Alifafanua kuwa wananchi 34 waliobaki ni wa awamu ya tano ambapo wanadai Sh. milioni 210 na walipaswa kulipwa mwaka wa fedha uliopita, lakini taratibu hazikukamilika hivyo watalipwa mwisho wa mwezi huu.

"Wananchi hawa kabla ya mwezi huu kuisha, fedha zao zitakuwa kwenye akaunti zao na malipo haya ni kipaumbele chetu kwa sababu tulifunga nao mwaka wa fedha uliopita," alisema.

**Ninafurahi kuona hawa wananchi 34 wanapata fidia hii na Halmashauri ya Jiji la Dodoma ninaipongeza kwa kutenga fedha hizo ambazo nimetaarifiwa zitalipwa mwezi huu.**

# Jafo aridhishwa ujenzi wa hospitali ya wilaya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Chamwino kuhakikisha unafikisha vifaa vya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru kwa wakati.

Akikagua ujenzi wake jana, Jafo alisema ameridhishwa nao na kuutaka uongozi huo kufikisha vifaa vinavyotakiwa kwa wakati ili ukamilike kwa mujibu wa mkataba. Waziri huyo pia alisisitiza kutumia malighafi za ndani kwa kuwa kuna viwanda vinavyozalisha vifaa vyenye ubora.

Alisema ndoto na wazo la Rais John Magufuli kujenga hospitali hiyo wilayani humo inakaribia kutimia.

**Ujenzi wa hospitali hiyo umefikia asilimia 82 na anahitaji wiki nne kuukamilisha.**

"Hapa palipofikia nimeridhika, nilikuwa ninatoka Morogoro, nilisimama hapa kukagua nikiwa kwa nje, jengo lilipofikia angalau ninapata amani maana hata ukiwa barabarani unaliona, na wote mnakumbuka tulikotoka tukiwa na kikwazi cha mvua kubwa," alisifu.

Aliipongeza Suma JKT kwa kazi waliyoifanya na kuzingatia utumiaji wa mfumo wa ununuzi wa 'force account'.

Mhandishi wa SUMA JKT, Omary Kabalagu, alisema ujenzi wa hospitali hiyo umefikia asilimia 82 na anahitaji wiki nne kuukamilisha.

Alisema mkataba ulitaka wamalize kujenga jengo hilo Agosti 23 mwaka huu, akifafanua: "Leo (jana) ni Agosti 18, unaona kabisa muda wetu uko chini ya siku 10, na kwa sasa tuko katika hatua ya umaliziaji."

Mhandisi huyo alisema tatizo lililopo ni kutofika kwa baadhi ya vifaa vya mifumo ya umeme, marumaru na maji.

"Endapo vikifika, basi ndani ya wiki nne tutakuwa tumekamilisha kabisa ujenzi huu," alisema.

Hospitali ya Uhuru inajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 3.99, fedha zilizotolewa na Rais Magufuli baada ya kuahirisha sherehe za maadhimisho ya Siku ya Uhuru Desemba 9, 2018 na zile zilizotokana na gawio la kampuni ya mawasiliano ya simu ya Airtel Tanzania.



Kinamama wachuuzi wa mboga wakifanya biashara kwenye daraja linalotumiwa na vyombo vya moto, nje ya Soko Kuu la Majengo, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# 'Wasimamizi uchaguzi watunze siri'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MSIMAMIZI wa uchaguzi Jimbo la Dodoma Mjini, amewataka wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi mkuu mwaka huu ngazi ya kata, kutunza siri na kuimarisha mawasiliano baina yao na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo, ili uchaguzi ufanyike kwa ufanisi.

Wakili Msekeni Mkufya alitoa rai hiyo jana jijini hapa alipowasilisha mada ya wajibu, majukumu na mambo ya kuzingatiwa na wasimamizi hao.

Alisema mambo yanayopaswa kuzingatiwa na wasimamizi wasaidizi wakati wa kutekeleza majukumu yao ni utunzaji wa siri ambazo alidai hazipaswi kutolewa kwa mtu au mamlaka zisizohusika.

"Mnatakiwa kutunza siri kwa maana ya kutokutoa taarifa za uchaguzi kwa mtu au mamlaka zisizohusika. Kuweka utaratibu mzuri wa kuwasiliana na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo, au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kuhusu mwenendo wa uchaguzi katika eneo lake," alisema.

Aliwataka kuacha ushabiki wa chama chochote cha siasa katika kutekeleza majukumu yao.

"Pia mnapaswa kukagua na kutembelea vituo vya uchaguzi vilivyopo katika maeneo yetu na mkibaini upungufu wa vituo, mtafute namna bora ya kurekebisha kasoro hizo kwa kuwasiliana na msimamizi wa uchaguzi," alisema.

Aliwataka kusimamia uchaguzi kwa kuzingatia uadilifu na uaminifu.

"Kwa sababu kukosea ni kuichafua Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kufanya jambo lolote kinyume cha sheria na kanuni za uchaguzi ni kosa, kifungu cha 98 cha Sheria ya Uchaguzi," alisema.

Msimamizi huyo aliwataka wasimamizi hao kuepuka kufanya kazi bila kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi au msimamizi wa uchaguzi.

"Kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi za mwaka 2020, inaelekezwa chini ya kanuni ya 13(1) kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaweza kuchagua ana kuteua wasimamizi wasaidizi kutoka miongoni mwa watumishi wa umma ambao watakuwa na jukumu la kumsaidia msimamizi wa uchaguzi katika jimbo na ngazi ya kata," alisema.





# Imani potofu chanzo uharibifu mazingira

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

IMANI potofu miongoni mwa jamii za wakazi wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, zimetajwa kuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira ikiwamo uchomaji ovyo wa misitu hali inayoathiri maisha ya viumbe hai.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la SALIOTA, linalotoa elimu ya uhifadhi wa mazingira wilayani hapa, Elisha Mwanikamwaga, aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya mwaka mmoja tangu lilipanzishwa.

Alisema utafiti ambao ulifanywa na shirika hilo, ulibaini kuwa katika wilaya hiyo kuna imani kuwa mtu akichoma moto misitu anakuwa na uwezo wa kuishi miaka mingi kuliko ambaye hajawahi kufanya tukio hilo.

Pia alisema baadhi ya wanajamii hao wana imani kuwa kuchoma misitu kunasaidia kupata mazao mengi mashambani na kuwakamata kirahisi wanyama wa porini kwa ajili ya kitoweo.

Alisema imani za aina hiyo ni za uongo na hazina faida yoyote kwa binadamu zaidi ya kuharibu mazingira ambayo ndiyo makazi ya viumbe hai wakiwamo wanyamapori, mimea, ndege na wadudu ambao wanapendezesha mazingira.

**Lakini kumekuwa na ongezeko kubwa la upandaji miti katika wilaya yetu jambo ambalo limekuwa na athari chanya za kimazingira. Tunategemea kama elimu hii itaendelea, utafika muda wilaya itakuwa ya mfano kitaifa.**

"Tuachane na imani za aina hiyo. Ukichoma msitu unaharibu vyanzo vya maji, unaua wanyamapori ambao pengine huwezi hata kuwala. Ndege watakufa na wengine watahama na kuna uwezekano mkubwa tukatengeneza jangwa ambalo litatutesa hata sisi," alisema Mwanikamwaga.

Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Mbarali, Raphael Shitindi, alisema elimu ya utunzaji wa mazingira ambayo inatolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imesaidia kupunguza tatizo la uharibifu wa mazingira wilayani humo.

Alisema kwa sasa kiwango cha uchomaji misitu ya asili kimeanza kupungua kutokana na wananchi kuanza kuelewa madhara ya matukio hayo na kwamba wameanza hata kuhamasishana kulinda misitu tofauti na ilivyokuwa awali.

Shitindi alisema mwaka jana walikuwa na matukio sita makubwa ya uchomaji moto misitu ya asili, lakini kutokana na elimu iliyotolewa, matukio hayo yamepungua na kufikia chini ya matukio manne.

"Lakini kumekuwa na ongezeko kubwa la upandaji miti katika wilaya yetu jambo ambalo limekuwa na athari chanya za kimazingira. Tunategemea kama elimu hii itaendelea, utafika muda wilaya itakuwa ya mfano kitaifa," alisema Shitindi.

Baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo walisema kutokana na elimu waliyoipata ya utunzaji wa mazingira, watahakikisha wanalinda mazingira hasa misitu ili waondokane na matatizo ambayo yamekuwa yakiwakabili ikiwamo ukosefu wa maji.

Mmoja wa wananchi hao, Ambokile Mwanyisi, alisema maeneo mengi yamekuwa yakikabiliwa na ukame hasa kipindi cha kiangazi hali ambayo inasababisha watumie muda mwingi kutafuta huduma hiyo.




Gari la mizigo aina ya Canter likiwa limesheheni viroba vya chupa tupu za plastiki katika eneo la Sinde, jijini Mbeya, jana. Ongezeko la viwanda vya kuchakata chupa hizo, limesababisha kupunguza uchafuzi wa mazingira jijini humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wadai kupigwa na waume kisa maji

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANAWAKE wa Kijiji cha Swaya wilayani Rungwe, wamedai kuwa ukosefu wa maji umekuwa ukiwasababishia vipigo kutoka kwa waume zao wanapochelewa kutoka kutafuta huduma hiyo.

Wakizungumza juzi na Nipashe kijijini hapo, wanawake hao walidai kuwa katika kijiji na kata nzima hakuna kijiji hata kimoja chenye maji ya bomba na hivyo wanategemea kutumia maji ya kwenye chemchemi ambayo pia ni madogo.

Mmoja wa wanawake hao, Sabina Mwalosi, alisema kutokana na tatizo hilo wanalazimika kutumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo na kwamba wamekuwa wakihisiwa na waume zao kuwa badala ya kuchota maji wao wanaenda kwa wanaume wengine.

"Wakati mwingine huwa tunarudi saa nne au saa tano usiku kutoka kwenye maji, lakini wanaume huwa hawaamini kuwa tulikuwa kwenye maji na badala yake huwa wanadhani tulikuwa kwenye michepuko kwa hiyo wanatupiga," alisema Sabina.

Alisema wananchi wa kijiji hicho walikubaliana kuchangishana fedha kwa ajili ya kuajenga mradi wa maji, lakini kutokana na tatizo la kiuchumi wameshindwa kuukamilisha hali ambayo inawafanya waendelee kupata shida.

Mwalosi aliiomba serikali kuwasaidia kukamilisha mradi huo ili waondokane na tatizo hilo ambalo linasababisha migogoro ya kifamilia ikiwamo kuvunjika ndoa.

Naye Tumpe George alisema uhaba wa maji kwenye eneo hilo unasababisha uhasama hata baina ya wanawake wenyewe kwa madai kuwa huwa wanagombana wanapochota maji hayo kwa kila mmoja kutaka atangulie kuchota.

Alisema endapo mradi wa kijiji utakamilika watakuwa wamekombolewa na kwamba watautumia muda wao mwingi kwenye shughuli za uzalishaji badala ya kutafuta huduma hiyo.

# RC atumbua viongozi wa chama cha madereva

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameuvunja uongozi wa Chama cha Madereva wa Malori ya Kubeba Mawe na Mchanga katika Jiji la Mbeya kutokana na kuwaongoza wenzao kimabavu ikiwamo kuwashinikiza kugoma kufanya kazi.

Aidha, ameliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata na kuwasweka ndani viongozi sita wa chama hicho ambao walihamasisha wenzao kugoma kubeba mawe kwenye mgodi wa mawe wa Nsalaga kwa siku nane kutokana na wachimbaji wa mawe kudai ongezeko la Sh. 5,000 ya bei ya mawe.

Akizungumza na madereva hao juzi katika eneo la mgodi huo, Chalamila aliwataja viongozi wa chama hicho ambao wanatakiwa kukamatwa kuwa ni Mawazo Mwashemele, Lwitiko Mwanyilu, Ambakuku Kyando, Yusuph Kazimoto, Samora Luoga na Petro Ngulo.

Chalamila alisema asilimia kubwa ya madereva hao walikuwa tayari kuendelea kufanya kazi na kulipia ongezeko hilo la Sh. 5,000 lakini walikuwa wanashindwa kufanya kazi kwa sababu ya shinikizo la viongozi wao.

"Nimekuja na lile gari (gari ya polisi) kwa ajili ya kuwabeba viongozi hao na ningewakuta hapa wangepigwa mkong'oto mpaka wakome. Sasa kwa vile hawapo hapa, namwagiza RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa), awasake popote walipo na hata kama watakimbilia mikoa mingine watapatikana tu," alisema.

"Endeleeni kufanya kazi mpaka mtakapochagua viongozi wengine. Leteni magari hapa yafanye kazi na RPC atawaweka vijana wake watasimamia ili yeyote atakayekuja kuwazuia aone kazi yake," aliongeza.

Alisisitiza kuwa hahitaji kusikia aina yoyote ya migomo ndani ya mkoa kwa maelezo kuwa anataka kujenga Mbeya yenye amani na utulivu na si yenye migomo ya ajabu ajabu.

Chalamila alisema kwa muda ambao mgomo huo umefanyika, mapato mengi yamepotea yakiwamo ya madereva, wamiliki wa malori, wachimba mawe pamoja na yale ya serikali.

Baadhi ya madereva ambao ni wanachama wa chama hicho, walimshukuru Mkuu wa Mkoa kwa uamuzi aliofanya kwa madai kuwa wamekuwa wakiteseka kwa muda mrefu bila kupata msaada wowote.

Mmoja wa madereva hao, Aman Kamwela, alisema viongozi hao walikuwa wanawatesa kwa kipindi kirefu na kwamba yeye mbali na kuwa dereva pia ni mmiliki wa magari, lakini viongozi waliyasimamisha kufanya kazi kwa wiki mbili.

## Wanawake 13 kugombea viti ubunge, uwakilishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAGOMBEA wanawake 13 wamepitishwa kugombea nafasi ya ubunge na uwakilishi kupitia Chama cha ACT-Wazalendo.

Kwa mujibu wa orodha ya wagombea wa CT-Wazalendo iliyotolewa, inaonyesha kwamba wagombea 13 wanawake wamepitishwa kuwania nafasi hizo kwa upande wa Unguja pekee.

Chama hicho hakijasimamisha wagombea wanawake kwa majimbo ya Pemba ambayo ndiyo ngome ya chama hicho, baada ya wafuasi wengi wa CUF kukihama kujiunga na ACT-Wazalendo.

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Elimu katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Zahara Ali Hamad, amepitishwa kuwania uwakilishi Jimbo la Dimani.

Naye Mwanamrisho Taratibu Abama amepitishwa kuwania nafasi ya ubunge katika Jimbo la Chumbuni, huku Mtumwa Ali Makame akiteuliwa kugombea Jimbo la Tumbatu.

Katika Jimbo la Malindi, Halima Ibrahim Muhamed, ameteuliwa kugombea baada ya kuwaangusha vigogo akiwamo aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Ali Saleh na Ibrahim Sanya ambaye katika mchakato wa kura za maoni, alishika nafasi ya kwanza.

Pavu Abdalla Juma amechaguliwa kuwania uwakilishi katika Jimbo la Donge, Mauwa Muhamed Mussa ubunge Jimbo la Shauri Moyo na Hidaya Yussuf ubunge Jimbo la Chwaka.

Wengine ni Aisha Mohamed Said (Tunguu), Sabahi Khamis (Paje), Raisa Abdallah Mussa (ubunge Mfenesini), na Thuwaiba Juma Uwakilishi jimbo la Mahonda.

**Pavu Abdalla Juma amechaguliwa kuwania uwakilishi katika Jimbo la Donge, Mauwa Muhamed Mussa ubunge Jimbo la Shauri Moyo na Hidaya Yussuf ubunge Jimbo la Chwaka.**

# Rais Shein ataja siri mafanikio uongozi wake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema Zanzibar imepata mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii kutokana na jitihada na uwezo wa viongozi na wananchi wake.

**Ofisi ilitangaza nafasi za ajira 5,083 katika utumishi wa umma Unguja na Pemba na kuanzisha Wakala wa Serikali Mtandao.**

Dk. Shein alisema hayo jana Ikulu Zanzibar, alipokutana na uongozi wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ulipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi kwa mwaka 2019/20 na mwaka 2020/21.

Alisema maendeleo makubwa ya kiuchumi yaliopatikana katika sekta mbalimbali, zikiwamo miundombinu na usafirishaji, upandishaji wa mishahara mara tano katika kipindi cha uongozi wake, ongezeko la pensheni na mambo mengine, yanayotokana na juhudi za serikali.

Mafanikio hayo, alisema yamewezesha kupungua kwa utegemezi wa bajeti ya serikali kwa asilimia tano hivi sasa.

Dk. Shein aliutaka uongozi wa ofisi hiyo kuandaa utaratibu wa kuwa na mipango ya mafunzo kwa watumishi wa serikali kwa kuzingatia mahitaji ya wizara husika na serikali kwa ujumla.

Aidha, aliwakumbusha viongozi na watendaji hao kuwa ofisi hiyo ni ya heshima, hivyo ni vyema pale wanapohitaji kuwaandikia barua watumishi kwa dhamira ya kubainisha muda wao wa kustaafu, wakazingatia lugha nzuri ikiwa hatua ya kuthamini mchango waliotoa katika kipindi kirefu cha utumishi wao.

Dk. Shein, aliuagiza uongozi wa ofisi hiyo kuweka kumbukumbu za muhtasari wa ongezeko la mshahara na ulipaji wa posho katika mashirika ya serikali na kusisitiza wajibu wa waziri kuwa ndio mwenye mamlaka ya kuidhinisha kiwango cha malipo hayo baada ya kupendekezwa na bodi.

Alisema pamoja na Chuo cha Utumishi wa Umma kuwa na azma ya kuendesha mafunzo ya uongozi, pia kinapaswa kuwa na mwelekeo wa mbali zaidi utakaolenga kukiimarisha na kukifanyia upanuzi, kama vile ujenzi wa hosteli kupitia mihula tofauti.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alisema pamoja na mafanikio makubwa yaliopatikana na ofisi hiyo, kutokana na kuwapo kwa uongozi bora, kuna dhana iliyojengeka miongoni mwa jamii kuwa ni vigumu kwa mwananchi kupata ajira serikalini hadi apate msukumo, huku taarifa zaidi zikihusisha baadhi ya watendaji kuuza ajira hizo.

Aliitaka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kuendelea kufanya kazi zake kwa umakini na weledi mkubwa ili kukabiliana na tatizo la rushwa ambalo serikali imekuwa ikipiga vita suala hilo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alimpongeza Rais Shein kwa busara na uadilifu mkubwa katika uongozi wake.

Alisema katika kipindi hicho ofisi hiyo ilitekeleza kwa mafanikio makubwa ikiwamo kuratibu na kuendesha mafunzo ya maandalizi ya kustaafu kwa watumishi 550 wa wizara, mashirika ya umma na taasisi mbalimbali zinazojitegemea.

Haroun alisema ofisi hiyo ilikamilisha uhakiki wa malipo ya mshahara na posho kwa wizara 13 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, idara na taasisi mbalimbali.

Aidha, alisema ofisi ilitangaza nafasi za ajira 5,083 katika utumishi wa umma Unguja na Pemba na kuanzisha Wakala wa Serikali Mtandao.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akimsikiliza Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee (katikati), wakati wa kikao cha Utekelezaji Mpango Kazi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, Ikulu jijini Zanzibar, juzi. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Gavu. **PICHA: IKULU**

## Balozi Iddi ataka juhudi kudhibiti mmomonyoko wa ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amezitaka taasisi zinazosimamia ujenzi wa miundombinu, manispaa, mazingira na serikali ya mkoa wa Mjini Magharibi, kuwa na mwelekeo wa pamoja utakaokuwa na njia sahihi ya muda mrefu kunusuru mmomonyoko wa ardhi katika fukwe za bahari.

Amesema ziko athari nyingi zilizojitokeza za uchafuzi wa mazingira katika sehemu mbalimbali za fukwe zikiwamo za maeneo ya Msuka na Mazizini ambayo kwa sasa hayako katika hali ya kuridhisha.

Balozi Iddi alisema hayo jana alipofanya ziara eneo la ufukwe wa Mazizini ambalo limeathirika vibaya kutokana na kupanda kwa kina cha maji ya bahari na kusababisha barabara iliyopita pembezoni mwa eneo hilo kumomonyoka.

Alisema jamii imekuwa ikishuhudia uchafuzi wa mazingira unaoongezeka sehemu tofauti nchini, licha ya baadhi ya maeneo kukumbwa na mabadiliko ya tabia nchi, lakini wakati mwingine husababishwa kwa makusudi na tabia za baadhi ya watu.

Balozi Iddi aliwataka viongozi pamoja na wataalamu wa taasisi hizo kuelewa kwamba wana dhamana ya kuhakikisha uchafuzi wa mazingira na mmomonyoko wa ardhi unamalizika au kupungua.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mustafa Aboud Jumbe, alisema serikali kupitia wizara hiyo, imeshatiliana saini mkataba na kampuni ya China inayojenga barabara ya Bububu hadi Mkokotoni kwa ajili ya ujenzi wa miradi mitatu itakayojengwa Zanzibar.

Jumbe aliitaja miradi hiyo kuwa ni mtaro wa maji machafu wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume, daraja ya Upenja kuelekea Kiwengwa na ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji ya bahari pembezoni mwa ufukwe wa Mazizini.

Alisema mradi huo wa ukuta utakwenda sambamba na bomba ya kupitishia maji machafu na ya mvua yanayotiririka kuingia pwani ya Mazizini ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi kwa mujibu wa ushauri wa wataalamu wa taasisi za mazingira.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mazingira Zanzibar, Sheha Mjaja, alisema katika kufanikisha suala hilo kuna haja ya kuwapo kwa timu maalum itakayopewa jukumu la kulinda eneo hilo kwa hatua ya kwanza ili kuzuia uvamizi wa kimazingira unaoweza kuharibu azma ya uimarishaji wa eneo hilo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA, Nyumba ya Gorofa 1, inauzwa na fremu za biashara, umeme na maji. Inafaa kwa kuishi na kwa biashara. Mawasiliano: 0757 079057.**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EMILY WILLIAM ELISHA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HIACE YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 594 DEP** YENYE CHASSIS NO **RZH1830002638** NA ENGINE **NO 2RZ88177** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

**TAARIFA YA POLISI; KAH/ RB/ 276/ 2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAUDA K MRISHO** amepotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SUNLG** yenye namba za usajiri **MC 749 AXW.** Yenye chassis namba **LBRSPJB57F9030163 na** Yenye rb namba **MOR/MOR/RB/601809/2020.**

115862102

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**RUMANYIKA SHABAN MSITA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA A GARI AINA YA DAF YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 877 CGU** NA TELLER LAKE LENYE NAMBA ZA USAJILI **T 634 CTC** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI **BGA /RB/1186/2020**

115862202

**THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR MBEYA AT MBEYA**

**APPLICATION No.67/2020**

**DORA ANTONY MASUNGWA::::::::::::::::::::::::::APPLICANT**

**Versus**

**NEEMA DISMAS MWITA::::::::::::::::::::::::::::1ST RESPONDENT**
**COPS AUCTION MALTA & :::::::::::::::::::::::::2ND RESPONDENT**
**COURT BROKERS LTD**

**SUMMONS TO FILE DEFENCE AND NOTICE FOR HEARING**

This is to inform the Respondents NEEMA DISMAS MWITA and COPS AUCTION MALTA AND COURT BROKERS LTD that the above case has been filed against you in this Tribunal.

**TAKE NOTICE THAT,** you have to file the Written Statement of Defence upon receipt of this notice.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT.I**n case the same is not filed immediately after receipt of this notice,the Tribunal will proceed to make necessary orders.
The case will come for mention on **19th day of August,2020.**
Given under my HAND and the SEAL of the Tribunal this 3rd day of August,2020.

T.Munzerere
TRIBUNAL CHAIRMAN
MBEYA

CHAIRMAN
TANZANIA

115862302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENEDICTA JAMES MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya Toyota **- IST** yenye namba za usajili no. **T897 CSA** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Polisi Taarifa:
**OB /RB/6073/2020**
**Simu na 0785580898**

## KUPOTEA KWA KADI

**SULEIMAN ABDALLAH OMARI** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI **MC 464 CLF** ILIYOTOLEWA NA MAMLAKA YA MAPATO. YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA CHA POLISI.
POLISI TAARIFA:
**TAN/TAN/RB/497043/2020**

## NOTISI YA KIMASLAHI

MIMI **OMARY RAMADHANI MSHANA** MTIA NAFASI YA UDIWANI KUPITIA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) KATA YA USA RIVER HALMASHAURI YA MERU MKOA WA ARUSHA NATANGAZA KUWA NI MKURUGENZI WA KAMPANI YA SHANENI ENTERPRISES LIMITED INAYOFANYA KAZI YA UKUSANYAJI USHURU WA USAFIRISHAJI WA MAZINGIZA NA HALMASHAURI YA MERU.

**IMETOLEWA LEO TAREHE 14.08.2020 NA MIMI OMARY R. MSHANA.**

SAHIHI.........................................

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Waganda wanne wawekewa vikwazo Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

WIZARA ya Fedha ya Marekani inayodhibiti mali za nchi hiyo Nje ya Nchi (OFAC), imewawekea vikwazo raia wanne wa Uganda, kufuatia amri ya kiutendaji.

Watu hao wameadhibiwa kwa kujihusisha na ulaghai wa malezi ya watoto, ambao umeshuhudia watoto waliozaliwa Uganda wakikabiliwa na madhila katika mikono ya waliokuwa wanaendesha mradi huu.

Alisema Marekani itaendelea na ahadi yake ya kuwatafuta na kuwafichua watu wote wanaokiuka haki za binadamu ulimwenguni.

Majaji wa Uganda Moses Mukiibi na Wilson Musalu Musene, Mawakili Dorah Mirembe, na Patrick Ecobu, walishiriki katika utapeli huo ambao katika mazingira fulani, watoto waliondolewa kutoka kwenye familia zao Uganda kwa ahadi ya kupatiwa elimu na kusoma Marekani, na hatimaye wakatolewa kwa familia za Marekani kuwalea.

Walipoondolewa kutoka kwenye makazi yao, wengi wa watoto hao waliwekwa katika nyumba iliyokuwa haina leseni ya kulea watoto mjini Kampala, na walifikishwa mahakamani na kutambulishwa kama kwamba wao ni yatima.

Wamarekani waliokuwa ndio walezi wa watoto hao bila ya kujua hilo waliwasili Uganda kuwachukua watoto hao ili kuwalea na kusafiri nao hadi Marekani. **VOA**

## UN yashutumu Idara ya Usalama wa Taifa Mali

**BAMAKO,** Mali

RIPOTI ya wataalamu wa Umoja wa Mataifa (UN), kuhusu Mali bado haijawekwa hadharani, lakini tayari imeitupia lawama Idara ya Usalama wa Taifa nchini humo.

Tofauti na zile zilizotangulia, zilizoyanyooshea kidolea cha lawama makundi yenye silaha, ripoti hii inawahusisha moja kwa moja viongozi kwa kuzuia kutekelezwa kwa makubaliano ya amani yaliyofikiwa mwaka 2015.

Wataalamu wanainyooshea kidolea cha lawama Idara ya Usalama wa Taifa na maofisa wake wakuu.

Wataalamu wa UN walisema kuwa Idara ya Usalama wa Taifa nchini Mali imekuwa chombo katika huduma ya mkakati usio rasmi.

Ripoti hiyo inabaini kwamba Idara ya Ujasusi ya Mali ilichochea mgawanyiko wa makundi kadhaa yenye silaha, hasa muungano wa CMA.

Ili kufikia hatua hiyo, SE iliunda kundi muungano mwingine na kuuita jina la CME mnamo mwaka 2017. Mohamed Ousmane Ag Mohamedoune anayeongoza muungano huo mpya, kulingana na ripoti hiyo, ni mmoja wa viongozi wanaolindwa na Idara ya Usalama wa Taifa. **RFI**

# Maaskofu Katoliki, chama cha wanasheria waikosoa Zimbabwe

**HARARE,** Zimbabwe

MAASKOFU wa Kanisa Katoliki na chama cha wanasheria nchini Zimbabwe, wameikosoa serikali kwa tuhuma za ukiukwaji wa haki za binadamu na ukamataji wa wapinzani.

Ukosoaji huo umeenda sambamba na wasi wasi juu ya namna serikali inavyowatendea wapinzani na mzozo mbaya wa kiuchumi.

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, alijibu kwa haraka sana, akisema tuhuma hizo mbaya zinazoelezewa hazina msingi wowote.

**Hali hiyo imefufua kumbukumbu za mfumuko mbaya wa bei chini ya utawala wa miaka 37 wa hayati Rais Robert Mugabe.**

Nchini Zimbabwe mfumuko wa bei umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 800, ikiwa ni dhahiri kwamba nchi hiyo inakabiliwa na mzozo mbaya wa kiuchumi katika kipindi cha muongo mmoja.

Hali hiyo imefufua kumbukumbu za mfumuko mbaya wa bei chini ya utawala wa miaka 37 wa hayati Rais Robert Mugabe, utawala uliomalizwa na mapinduzi ya kijeshi mwaka 2017.

Maaskofu walisema katika barua yao kwamba Zimbabwe inakabiliwa na mfululizo wa mizozo, ikiwamo uchumi kudorora, umaskini uliokithiri, rushwa na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Akijibu barua hiyo ya maaskofu wa Kanisa Katoliki, Waziri wa Habari, Monica Mutsvangwa, alikosoa kiongozi wa mkutano wa maaskofu Katoliki Robert Ndlovu, na kuielezea barua ya maaskofu hao kama ujumbe wa kishetani, wenye lengo la kuchochea mauaji wa halaiki kama yaliotokea nchini Rwanda.

Wakosoaji wanamshtumu Rais Mnangagwa, ambaye alikuwa Makamu Rais wa Robert Mugabe, kwa kutumia mifumo ya kidikteta kama ile iliyoshuhudiwa wakati wa utawala wa mtangulizi wake. **VOA**




Raia wa Zimbabwe wakiandamana nje ya ubalozi wa nchi yao, mjini London Uingereza wakipinga kukithiri kwa ufisadi nchini mwao. **PICHA: VOA**

# Kamatakamata yaibua hofu Ethiopia

**ADDISABABA,** Ethiopia

TUME ya Haki za Binadamu nchini Ethiopia imesema vyombo vya dola nchini humo vimewakamata watu zaidi ya 9,000 baada ya makabiliano makali yaliyozuka mwezi uliopita.

Taarifa hizo zimezidisha wasiwasi kuwa serikali ya Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, iliyosifiwa kwa kuleta mageuzi inarejesha enzi ya kutumia mbinu katili na za mkono wa chuma za tawala zilizotangulia.

Abiy aliyeingia madarakani mwaka 2018, kwa ahadi ya mageuzi ya kisiasa katika moja ya mataifa yenye rekodi dhaifu kwa ukandamizaji barani Afrika, hivi sasa anakabiliana na uasi uliojitwika nembo ya ukabila ambao sasa umegeuka kuwa vurugu.

Mabadiliko yanayosimamiwa na Abiy, yamefufua mizozo ya enzi na enzi kuhusu umiliki wa ardhi, rasilimali na hata madaraka katika ngazi ya chini ya utawala na sasa anakabiliwa na changamoto ya kuwalinda raia, huku akitetea misingi ya uhuru na haki za wengine iliyomwezesha kushinda Tuzo ya Amani ya Nobel mwaka uliopita.

Mwanasiasa huyo kijana aliahidi Ethiopia itafanya uchaguzi huru na wa haki ifikapo mwaka 2021, utakaokuwa na mafanikio muhimu katika Taifa hilo la pili kwa idadi ya watu barani Afrika.

Hata hivyo, Tume ya Haki za Binadamu nchini humo imesema watu 9,000 wamekamatwa tangu shambulizi la bunduki lililomuua mwanamuziki mashuhuri nchini humo, kuzusha maandamano yaliyosababisha vifo vya watu 178 kwenye mji mkuu Addis Abbaba na maeneo jirani.

Vurugu hizo ni mbaya kuwahi kushuhudiwa tangu Waziri Mkuu ABiy, alipoingia madarakani.

Serikali ilipotakiwa kutoa ufafanuzi wa taarifa hizo imeonyesha kuwa kurejesha utulivu ndiyo kipaumbele cha hivi sasa.

Msemaji wa Waziri Mkuu, Billene Seyoum, alisema kuwa moja ya wajibu wa msingi wa serikali ni kuhakikisha usalama na uthabiti wa utawala wa sheria, kwamba hatua ambazo serikali imekuwa ikichukua wiki chache zilizopita zinadhihirisha nia yake ya kuimarisha utii wa sheria na katiba. **DW**




# KOMPANY ASTAAFU SOKA, SASA KOCHA ANDERLECHT

**BRUSSLES,** Ubelgiji

VINCENT Kompany amestaafu kucheza soka katika umri wa miaka 34, na ametajwa kuwa kocha mkuu wa Anderlecht.

Nyota wa zamani wa kikosi cha Ubelgiji aliteuliwa kuwa kocha mchezaji Mei mwaka 2019 baada ya kuondoka Manchester City.

Ripoti zimebainisha kwamba, Kompany, amekubali kusaini mkataba wa miaka minne na kikosi hicho.

"Vincent ni kocha mpya wa RSC Anderlecht. Na atakuwa hapa kwa misimu minne ijayo," ilisomeka taarifa hiyo kutoka Anderlecht.

"Ameacha kucheza na sasa majukumu yake mapya ni kuwa kocha mkuu wa kikosi chetu."

Kompany alicheza kwa kipindi cha miaka 11 akiitumikia Man City akiwa nahodha na aliisaidia kubeba mataji matatu msimu wa 2018-19.




# *Mikel ajiunga Stoke City*

**LONDON,** England

KIUNGO wa zamani wa Chelsea, John Obi Mikel, amesajiliwa na timu ya Daraja la Kwanza ya Stoke City.

Nahodha huyo wa zamani wa Nigeria alitumia msimu wa 2018-19 akicheza na timu ya Middlesbrough kabla ya kujiunga na miamba wa Uturuki, Trabzonspor.

Hata hivyo, Mikel aliondoka klabuni hapo Machi mwaka huu baada ya kupinga ligi hiyo kuendelea kuchezwa wakati kuna mlipuko wa virusi vya corona.

Yeye ni usajili wa nne kwa Stoke baada ya kusajiliwa kwa Morgan Fox, James Chester na Steven Fletcher pale kwenye Uwanja wa 365.

"Tunafurahi kumleta John klabuni kwetu. Bado kiwango chake kinaongea na ni aina ya mchezaji anayeweza kuisaidia timu," alisema kocha, Michael O'Neill.

"Tulitumia saa nne kuzungumza naye na alibainisha kwamba anataka kurudi kwenye Ligi Kuu na kumaliza kipindi chake cha uchezaji."

Mikel alishinda mataji mawili ya Ligi Kuu, matatu ya FA na Ligi ya Mabingwa msimu wa 2011-12 wakati akicheza pale Chelsea.

Ameichezea timu ya Taifa ya Nigeria mechi 91, akicheza kwenye michuano ya Kombe la Dunia mara mbili na alitwaa taji la michuano ya Kombe la Afrika mwaka 2013 kabla ya kutangaza kustaafu kuichezea timu ya taifa.

# Koeman ni muda tu kocha mpya Barca

**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman anajipanga kuwa kocha mkuu mpya wa Barcelona, kwa mujibu wa uvumi ulioenea nchini Hispania.

Quique Setien alifukuzwa na Barcelona Jumatatu, baada ya klabu hiyo kukumbana na kipigo cha aibu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na kocha huyo wa timu ya Taifa ya Uholanzi, Koeman na mlinzi wa zamani wa Barca, ameripotiwa kwamba yupo kwenye nafasi nzuri ya kuteuliwa kuwa kocha mpya.

Koeman ameripotiwa kwamba, ndiye mtu anayetakiwa pale Barca na kwamba wanataka kumfanya kuwa mrithi wa Setien. Barcelona iliondolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali na Bayern Munich kwa kufungwa mabao 8-2.

Lakini Barcelona msimu huu imeondoka mikono mitupu baada ya kupokonywa taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga na wapinzani wao, Real Madrid.

Gazeti la Marca na Sport liliandika jana Jumanne kuwa Koeman atatangazwa wakati wowote kuwa kocha mpya wa Barcelona.



HABARI MICHEZO

# Martinez: Inter ipo tayari kubeba taji la Europa

**DUSSELDORF,** Ujerumani

LAUTARO Martinez amesema Inter Milan ipo tayari kwa kupata mafanikio makubwa zaidi baada ya kuwaondoa Shakhtar Donetsk na kutinga fainali ya Kombe la Ligi ya Europa.

Martinez na Romelu Lukaku kila mmoja alifunga mara mbili wakati kikosi hicho cha kocha, Antonio Conte kikitoa kichapo kikali kwa Shakhtar cha mabao 5-0 mjini Dusseldorf.

Danilo D'Ambrosio pia alifunga bao moja kwa Inter, ambapo walitinga fainali ya Ulaya kwa mashindanoya Ulaya kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2010, wakati waliposhinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakishinda mataji matatu chini ya kocha, Jose Mourinho.

Martinez ambaye anawaniwa na Barcelona, alibainisha baada ya mchezo huo akiiambia Sky Sport Italia: "Ulikuwa usiku wa aina yake, kitu ambacho tulikuwa tunakiona muda mrefu.

"Umepita muda mrefu tangu nilivyocheza vizuri namna ile, na kwenye nusu fainali tulijiimarisha kwamba Inter ipo tayari kwa vitu vikubwa. Tupo tayari kwa fainali.

"Mabao haya yametupa sisi kitu fulani, tuliamini kwamba mchezo ule utakuwa muhimu, lakini tulipata matokeo rahisi.

"Na kwa sasa timu inaonekana kuimarika zaidi na zaidi nina furaha kubwa kuwa sehemu ya kikosi hiki na kutoa mchango wangu mkubwa."




# BARCA WAMTEMA RASMI SETIEN



**BARCELONA,** Hispania

QUIQUEN Setien amefukuzwa rasmi kama kocha wa Barcelona baada ya kukumbana na kichapo kikali kutoka kwa Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kichapo cha Ijumaa iliyopita cha mabao 8-2 kwenye robo fainali mjini Lisbon kimeiweka rehani nafasi ya Setien pale Barca.

Na juzi bodi ya klabu hiyo iliamua kuachana rasmi na kocha huyo mwenye umri wa miaka 61, ambaye amehudumu kwenye nafasi hiyo kwa kipindi cha miezi saba, huku kocha wa Uholanzi, Ronald Koeman akitarajiwa kuchukua nafasi yake.

"Bodi ya Wakurugenzi imekubaliana kwamba, Quique Setien hataendelea kuwa kocha wa kikosi cha kwanza," taarifa ya klabu hiyo ilieleza.

"Hii ni hatua ya kwanza kwa bodi wakati tukiwa kwenye harakati za kujenga upya timu na kocha mpya atatangazwa ndani ya siku chache zijazo."

Barca pia walipoteza nafasi ya kutetea taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga wakati alipoliachia kwa wapinzani wao Real Madrid.

# *Silva atua Sociedad, kujengewa sanamu*

**MADRID,** Hispania

DAVID Silva amerudi kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, baada ya kuondoka Manchester City, akisajiliwa Real Sociedad kwa uhamisho huru.

Kipindi cha miaka 10 akicheza kule City, kilimalizika Jumamosi baada ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Lyon na Silva alionekana kwamba anaelekea kwa miamba wa Serie A, Lazio.

Hata hivyo, Sociedad ilifanikiwa kupata saini yake, huku Silva ambaye aliondoka Valencia mwaka 2010 kuendeleza kipaji yake England - akiamua kurudi nyumbani.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu, matano ya EFL na FA mara mbili wakati akicheza pale City, amekubali kusaini mkataba wa miaka miwili na klabu hiyo ya Basque.


Sociedad, ambao wamempa Silva jezi namba 21, walimaliza nafasi ya sita kwenye msimamo wa LaLiga msimu wa 2019-20, ingawa walishinda mechi mbili tu kati ya 11 baada ya msimu kurudi tena.

Walitinga fainali ya Kombe la Copa del Rey Machi, ingawa mechi hiyo haikuchezwa kwa sababu Sociedad na wapinzani wao Athletic Bilbao, kukataa kuingia uwanjani hadi hali ya kiafya iwe salama baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

Jumatatu, City ilibainisha kwamba itamjengea sanamu ambayo itakuwa kwenye Uwanja wa Etihad.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DE GEA: NITABAKI NAMBA MOJA UTD

●●● Najiamini mwenyewe, nimeonyesha ubora wangu kwa miaka yote, hivyo nitaendelea...

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, David de Gea amesema anajiamini yeye mwenyewe kuendelea kuwa golikipa namba moja wa klabu hiyo, wakati uvumi ukikua kuhusu majaliwa yake.

**De Gea amekuwa akishutumiwa kwa msimu wa 2019-20 kwa kutokuwa kwenye kiwango bora, huku makosa yake yakichangia United kuondolewa na Chelsea kwenye robo nusu fainali ya Kombe la FA, katika Uwanja wa Wembley mwezi uliopita.**

Kiwango cha Dean Henderson akiwa anacheza kwa mkopo kule Sheffield United kimeibua maneno ya mashabiki kutaka Muingereza huyo arudi pale Old Trafford ili kutoa changamoto kwa De Gea.

Lakini De Gea, ambaye ameshinda taji la Ligi Kuu, Kombe la FA, Ligi ya Europa, EFL na Ngao ya Jamii tangu awasili hapo akitokea Atletico Madrid mwaka 2011, anajiamini kwamba ana uwezo wa kuonyesha kiwango cha juu zaidi pale United.

"Najiamini mwenyewe," alisema De Gea - ambaye mkataba wake na United unamalizika Juni 2023.

"Nimeonyesha ubora wangu kwa miaka yote, hivyo nitaendelea kuwa hapa kwa kocha yoyote.

"Mara zote nipo tayari kucheza na kujaribu kuisaidia timu kama ambavyo nimekuwa nikifanya."

Msimu wa United ulimalizika kwa machungu zaidi Jumapili iliyopita baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Sevilla kwenye robo fainali ya Kombe la Europa.

Ilikuwa ni nusu fainali ya tatu kwa United kupoteza msimu huu baada ya kutolewa kwenye Kombe la FA na lile la EFL.

Kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskjaer hata hivyo kilifanikiwa kumaliza kwenye nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

"Nafikiri tumeimarika msimu huu," alisema golikipa huyo wa kimataifa wa Hispania, De Gea.

"Tulikuwa tumepitwa pointi 14, lakini tulimaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu."

## ZISIKUPITE

### CITY WAMRUDIA KOULIBALY

KLABU ya Manchester City imefufua tena azma yake ya kutaka kumsajili mlinzi wa Napoli raia wa Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, baada ya kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(La Repubblica via Talksport)***

### HATIHATI KUMKOSA KAI

KLABU ya Chelsea imearifiwa kwamba inahitajika kulipa pauni milioni 90 au ikabiliwe na tishio la kumkosa mchezaji wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 19. ***(Standard via Daily Star)***

### YAJIPANGA KWA NEYMAR

BARCELONA ipo tayari kuanzisha jaribio la kumsajili tena Neymar kutoka Paris St-Germain, wakati ikiwa mbioni kujiimarisha baada ya kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mail)***

### SANCHO AKOMALIWA

MKURUGENZI Mtendaji wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke amedai klabu hiyo haiko chini ya shinikizo lolote la kumuuza mlengwa wa Manchester United Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, licha ya mahesabu kuonyesha hasara ya pauni milioni 39.8 kwa kipindi cha mwaka hadi Juni 30, mwaka huu. ***(Manchester Evening News)***

### UNITED WAMTAKA COSTA

MANCHESTER United inamfuatilia kwa karibu winga wa Brazil na Juventus, Douglas Costa mwenye umri wa miaka 29, inapoanza safari yake ya usajili wa msimu mpya. ***(Sky Sports)***

### YAKATAA BEI YA ALCANTARA

LIVERPOOL bado ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Bayern Munich, Thiago Alcantara, lakini imeiarifu klabu hiyo ya Bundesliga kuwa haiko tayari kulipa pauni milioni 27.2 kwa raia huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake umesalia mwaka mmoja. ***(Guardian)***

### BENFICA YAMUWANIA CAVANI

KLABU ya Benfica ya Ureno inaonekana kuiongoza Leeds United katika kinyang'anyiro cha kumsajili nyota wa Paris St-Germain raia wa Uruguay, Edison Cavani huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, akiwa anapatikana kwa uhamisho wa bure. ***(Goal)***

### CAICARA AGOMBEA ENGLAND

KLABU ya West Brom na West Ham zimearifiwa kwamba kitita cha karibu pauni milioni 2.7 kitahitajika kumsajili beki wa Istanbul Basaksehir na Brazil, Junior Caiçara mwenye umri wa miaka 31. ***(Sport Witness via Birmingham Mail)***

### NUNEZ AWANIWA EPL

BRIGHTON na Sheffield United ni miongoni mwa klabu zinazomwania mshambuliaji wa Almeria na Uruguay, Darwin Nunez huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, akitaka malipo ya karibu pauni milioni 14 kwa mwaka. ***(Talksport)***

### AMPADU AMTEGA LAMPARD

KINDA wa Chelsea, Ethan Ampadu mwenye umri wa miaka 19, ambaye msimu uliopita alikuwa RB Leipzig kwa mkopo, anajitahidi kumridhisha Frank Lampard huku ikiaminika kuwa kocha huyo ni shabiki wake. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

## Azam: Usajili huu ni wa ubingwa

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukamilisha usajili wa mshambuliaji kutoka Highlanders FC ya Zimbabwe, Prince Dube, Klabu ya Azam FC imesema usajili wanaoufanya msimu huu, wanauhakika wa kwenda kutoa upinzani wa mbio za ubingwa dhidi ya Simba inaoushikilia, lakini pia Yanga ambayo inaonyesha kuupania.

Azam juzi ilikamilisha usajili wa Dube, ambaye anakuwa mchezaji wa sita kusajiliwa na timu hiyo baada ya kipa David Kisu, beki wa kushoto Emmanuel Charles, kiungo mkabaji, Ally Niyonzima na viungo washambuliaji Awesu Awesu na Ayoub Lyanga.

Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin `Popat` aliliambia Nipashe jana kuwa, kuelekea msimu mpya wa 2020/21 unaotarajiwa kuanza Septemba 6, mwaka huu, wanataka kula sambamba na Klabu za Simba na Yanga kuusaka ubingwa na kuirudisha timu ya msimu wa 2013/14 iliyotwaa kombe hilo.

Alisema wamefanya mabadiliko makubwa katika usajili wao kwa kuimarisha kikosi chao katika nafasi mbalimbali ikiwamo kujiimarisha zaidi katika safu ya ushambuliaji ambayo msimu ulioisha ilikuwa na changamoto kubwa ya kuziona nyavu.

"Msimu huu unaoanza Azam tunajambo letu, tumesajili kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi, kuhakikisha tunairejesha Azam dume ambayo ilitwaa ubingwa msimu wa 2013/14," alisema.

## Gwambina kwa kipa Mzambia

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Gwambina FC yenye maskani yake Misungwi, Mwanza, umesema unatarajia kusajili mlinda mlango kutoka nchini Zambia kwa ajili ya kuiongezea nguvu timu hiyo, ambayo imepanda daraja msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu kutoka Misungwi, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Fulgence Novatus aliweka wazi kuwa mazungumzo na mchezaji huyo yanaendelea vizuri ni kudai ni mmoja wa makipa wenye historia nzuri kisoka.

"Huyo mlinda mlango yupo njiani, mpaka kesho mchana kila kitu tutakiweka wazi, kwa sasa siwezi kukupa uhakika mpaka hapo atakapofika kama tukikubaliana naye ninaamini tutakuwa tumepata mchezaji bora katika kikosi chetu," alisema Novatus.

Aidha, alisema wachezaji ambao amewasajili msimu huu wanaonyesha ushindani mkubwa mazoezini jambo ambalo amekiri kumpa matumaini makubwa kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu, ambapo wataufungua kwa kuanzia ugenini dhidi ya Biashara United ya Mara.

# CLASSIC, NASSIB KUWAKARIBISHA DULLA MBABE, KIDUKU ULINGONI

**Na Mwandishi Wetu**

PAMBANO kati ya Twaha Kiduku na Dulla Mbabe kuwania ubingwa wa Taifa wa uzito wa Kati (Super Middle), ambalo litakuwa la raundi 12, litaanza kwa kukaribishwa na bondia aliye katika kiwango cha juu nchini, Ibrahim Classic atakapopanda ulingoni kuvaana na Nassib Ramadhan, imeelezwa.

**Mabondia hao watapambana Agosti 28, mwaka huu katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, na tayari maandalizi yamekamilika kwa mujibu wa mratibu wa pambano hilo, Jay Msangi.**

Akizungumza na mwandishi wetu, Msangi alisema siku hiyo kutakuwa na mapambano ya utangulizi sita; akiyataja mengine kuwa ni kati ya Halima Vunjabei dhidi ya Agness Kayanje wakati Habib Pengo akivaana na Johncena Ramadhan, huku Paul Kamata akiwa na kibarua kigumu dhidi ya Hussein Mutaba.

"Pambano hilo kati ya Dulla na Twaha litakuwa ni la kikabila, litakwenda kuamua nani atakuwa mbabe wa Wazaramo," alisema Msangi.

Mratibu huyo alisema viingilio vya pambano hilo vimebadilika baada ya Kampuni ya GSM kujitokeza kudhamini pambano hilo na kwamba sasa kiingilio cha juu ambacho awali kilikuwa Sh. 100,000 sasa mashabiki watalipia Sh. 50,000 huku cha chini ambacho ni Sh. 10,000, kikipatikana kwa Sh. 5,000 kwa atakayenunua tiketi yake mapema.

Alisema mabondia wote watapima uzito na afya Agosti 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kinesi ulioko Shekilango jijini.

Aliongeza kuwa, pia kutakuwa na pambano la "show off" ambalo litahusisha mabondia chipukizi wenye umri wa miaka tisa, huku akisisitiza ulinzi na usalama utakuwa wa kiwango cha juu.

Naye Ofisa Biashara Mkuu wa GSM, Allan Chonjo, alisema wameamua kuwa sehemu ya pambano hilo ili kuendelea kushiriki katika kukuza michezo hapa nchini.




Meneja mashindano wa Klabu ya Simba, Hamisi Kissiwa, akizungumza na waandishi wa habari kwenye hafla ya kukabidhi jezi na vifaa vya michezo kwa timu za Dar City FC na Tandale FC katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja Uhusiano SportPesa, Sabrina Msuya. **PICHA: SPORTPESA**

# *SportPesa, Simba wagawa vifaa vya michezo*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo na Burudani SportPesa kwa kushirikiana na Klabu ya Simba imegawa vifaa vya michezo kwa timu mbili jijini Dar es Salaam kuelekea maadhimisho ya Wiki ya Simba 2020 chini ya udhamini wa SportPesa.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Meneja Uhusiano SportPesa, Sabrina Msuya alisema wamegawa vifaa vya michezo kwa timu mbili ambazo zimependekezwa na uongozi mzima wa Simba kuelekea kilele cha "SportPesa Wiki ya Simba".

"Lengo letu kuu kama wadhamini wakuu wa timu hii ni kukuza na kuendeleza michezo nchini hasa mpira wa miguu na ndio maana tumesaidia hizi timu zinazoshiriki Ligi Daraja la Tatu ili kuweza kuwainua kwa namna moja ama nyingine.

"Tandale FC na Dar City FC tumeanza nao msimu huu, zoezi hili ni endelevu, kwa mwaka jana tulikaribisha msimu mpya wa Simba kwa kusaidia timu tatu kutoka Wilaya ya Kinondoni, Ilala pamoja na Temeke.


Kwa upande wa Meneja Mashindano wa Klabu ya Simba, Hamisi Kissiwa, aliongeza, wamefurahi sana kuungana na SportPesa katika kuadhimisha na kuzisaidia timu hizo.

"SportPesa mnaweza mkaona huu ni msaada mdogo, lakini kusema ukweli mnaenda kuwainua sana na kuwafanya wafikie ndoto yao," alisema Kissiwa.

Katibu Mkuu wa Dar City FC, Rajabu Samora, yeye alisema: "Tunaishukuru sana Kampuni ya SportPesa kwa kutuona na kutambua mchango wetu kwenye mpira, kwani tunapitia changamoto mbalimbali na leo wamedhihirisha kwa kutupatia vifaa vya michezo."

Baada ya makabidhiano hayo wachezaji wa timu hizo walifanya mazoezi kuonyesha umati uliokuwa ukishuhudia makabidhiano hayo, wakionyesha uwezo wao uwanjani hapo.


Michezo
Jumatano Agosti 19, 2020
Nipashe



De Gea: Nitabaki namba moja UTD

UKURASA 22

SASA SUBIRINI...



Mkurugenzi Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, Mhandisi Hersi Said, ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Klabu ya Yanga, akiwa na kiungo mkabaji, Mukoko Tonombe (kushoto), pamoja winga Tuisila Kisinda (kulia), baada ya kumalizana na klabu yao ya AS Vita ya Kinshasa, DR Congo na wachezaji hao kumwaga wino. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simba, Vital'O vitani Simba Day

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetangaza rasmi kuwa itacheza dhidi ya Vital'O ya Burundi kwenye Tamasha lake la kila mwaka la Simba Day, ambalo mwaka kuu linajulikana kama Wiki ya Mabingwa.

Taarifa za klabu hiyo kupitia mtandao wao rasmi jana zilieleza kuwa timu hiyo ya zamani ya wachezaji Ladit Mavugo na Amissi Tambwe ambao wote wameshawahi kuichezea Simba, ndiyo watakayocheza nayo Jumamosi ijayo, Agosti 22 kwenye Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam.

"Nyasi za Uwanja wa Mkapa zitawaka moto kwenye 'Simba Day' 2020 kwa kuwakabili Vital'O kutoka nchini Burundi," ilieleza taarifa hiyo.

Simba Day ni tamasha la kila mwaka kwa klabu hiyo ambalo kutumika kutambulisha jezi rasmi za klabu hiyo, pamoja na wachezaji wote wa msimu mpya, ikicheza mechi na timu moja kutoka nje ya nchi, pamoja na burudani nyingine za soka na muziki.

Mbali na wachezaji wa zamani, wapya watakaotambulishwa siku hiyo ni Ibrahim Ally Ame kutoka Coastal Union, Charles Ilamfya (KMC), David Kameta (Lipuli FC), Larry Bwalya na Chriss Mugalu kutoka Power Dynamos ya Zambia, Joash Onyango (huru) aliyemaliza mkataba na Gor Mahia ya Kenya na Benard Morrison (huru) baada ya kumaliza mkataba na Yanga.

Tamasha hilo lilianzishwa mwaka 2009 na aliyekuwa Mwenyekiti wa klabu hiyo wakati huo, Hassan Dalali ambapo kwa mara ya kwanza ilicheza dhidi ya SC Villa ya Uganda na kushinda bao 1-0.

# KOCHA MPYA YANGA MZIGONI KIMYA KIMYA

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Ni Mrundi Cedric Kaze, wachezaji wamwagiwa dozi ya kutosha, sasa kutambulishwa...

WAKATI mashabiki wa Klabu ya Yanga wakisubiri kwa hamu kumjua na kumuona kocha mkuu wa kikosi hicho, mazoezini tayari wachezaji wa timu hiyo wameanza kuzifaidi mbinu na mfumo wa kocha huyo ambaye atatambulishwa rasmi mwishoni mwa wiki hii, imefahamika.

**Yanga ambayo kwa muda mrefu imekuwa sokoni kutafuta kocha mkuu wa kurithi mikoba ya Mbelgiji Luc Eymael aliyetimuliwa baada ya kumalizika msimu wa 2019/20, imeanza mazoezi ikiwa chini ya Kocha wa viungo, rai wa Afrika Kusini, Riedoh Berdien.**

Ingawa mashabiki wa soka wamekuwa wakishangaa na kuhoji usajili unaofanyika bila kocha ikiwa ni pamoja na mazoezi yanayoendelea, lakini habari za uhakika ni kwamba tayari kocha mkuu wa kuinoa timu hiyo ameshapatikana na kuanza kazi kwa kutuma programu ambazo zinatumiwa mazoezini na msaidizi wake, Berdien.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Wakili Simon Patrick, amewataka Wanayanga kutulia huku akiwaeleza kila kitu kinakwenda vizuri ikiwa ni pamoja na kocha huyo kuanza kazi kwa kutuma progamu zake ambazo zinatumika mazoezini kwa sasa.

"Wiki hii watajua kila kitu, na kuhusu mazoezi, tayari ametuma progamu zake ambazo wachezaji wanaendelea nazo kupitia kwa kocha msaidizi," alisema Simon.

Lakini kwa upande wa Mkurugenzi Mwekezaji ndani ya GSM, Injinia Hersi Said, wanaoidhamini Yanga kupitia kampuni hiyo na ambao wamekuwa mstari wa mbele katika suala nzima la usajili wa wachezaji pamoja na kutafuta kocha, naye alisema atatangazwa rasmi ndani ya wiki hii, Alhamisi ama Ijumaa.

Hersi alisema tayari wamempata kocha wa kukinoa kikosi hicho na kwa sasa anasubiri vipimo vya corona (COVID-19) kutoka ili kuweza kupata kibali cha kusafiri.

Alipotajiwa jina la Mrundi Cedric Kaze, anayetajwa kuwa ndiye atakayekinoa kikosi hicho, Hersi alisema "haupo mbali" huku akieleza kwamba kwa sasa kocha wao yupo Amerika Kusini.

"Kilichomchelewesha kutua ni kutokana na kusubiri vipimo vya COVID-19, lakini kati ya Alhamisi (kesho) ama Ijumaa anaweza kuwasili na tutamtangaza rasmi, hivyo Wanayanga wasubiri mambo mazuri yanakuja," alisema.

Kuhusu usajili wa timu hiyo, baada ya juzi kuwanasa viungo wawili kutoka AS Vita ya DR Congo, Mukoko Tonombe na Tuisila Kisinda, Hersi alisema wanafanya usajili makini ambao utawafanya Wanayanga kukaa jukwaani wakinywa kahawa huku wakishuhudia timu yao ikishinda mabao manne ama matano.

"Kwa hapa Congo suala la usajili tumemaliza, tunahamia nchi nyingine, bado tunahitaji mshambuliaji mmoja wa boksi kwa boksi atakayetufanya kuwania ubingwa," alisema Hersi akiwa Congo alipokwenda kukamilisha usajili wa viungo hao.

Kisinda ambaye ni winga na Mukoko anayecheza nafasi ya kiungo mkabaji lakini pia akiwa na uwezo wa kucheza kama kiungo mshambuliaji, ni miongoni mwa wachezaji waliokuwamo katika kikosi cha AS Vita kilichoipiga Simba mabao 5-0 DR Congo kabla ya kuja nchini na kuchapwa 2-1 katika Uwanja wa Taifa (kwa sasa Mkapa) kwenye mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka jana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >